SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

**RIPOTI MAALUM**
Mapenzi yanavyochochea kasi magonjwa ya akili



UKURASA 5






Pambana joto lisiharibu ngozi yako

Jumapili Novemba 21, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • No. 0580771
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Ahueni makali mgawo yanukia

**Kina** cha maji chaongezeka Ruvu, siku moja baada ya raia wa China kubambwa, RC atoa maagizo mazito... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan, akipokea zawadi ya ngalawa kutoka kwa Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Zanzibar, Swahiba Kisasi wakati wa mkutano ulioandaliwa na jumuiya hiyo, kwa ajili ya kumpongeza katika Viwanja vya Maisara Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

## Samia: Naona fahari, napata ari, ujasiri kuniunga mkono

UKURASA 2



## HOTELI NNE ZA KITALII ZATEKETEA KWA MOTO

UKURASA 3

Moto ukiteketeza hoteli nne za kitalii katika eneo la Jambiani, Mkoa wa Kusini Unguja juzi jioni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**MICHEZO** SIMBA YAFUNGUKA ILIVYOIMALIZA RUVU UK.24 | **MAONI, KATUNI** UK.6

## Serikali yapewa dawa za malaria zilizotelekezwa

**Na James Kandoya**

SERIKALI imepokea dozi 125,520 za dawa ya kutibu ugonjwa wa malaria aina ya ALU zenye thamani ya Sh. milioni 51.8 ambazo zimetolewa na Mamlaka ya Mapato (TRA) baada ya mfanyabiashara mwenye dawa hizo kutojitokeza kuchukua mzigo wake bandarini.

Akipokea dawa hizo kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, jana jijini Dar es Salaam, Mfamasia Mkuu wa Serikali, Daudi Msasi, alisema dawa hizo zimeshafanyiwa uchunguzi na mamlaka husika na zinafaa kwa matumizi ya binadamu. Alitaja dozi zilizopokewa za watu wazima ambazo ni tani tatu na kwamba zitaenda kugawiwa katika vituo vyote vya afya nchini ili kuwasaidia wananchi katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa malaria.

"Tunawashukuru sana TRA kwa kuona umuhimu wa kusaidia jamii kama ambavyo wamekuwa wakifanya kuhakikisha tunakuwa katika nafasi moja pindi jamii inavyokumbwa na ugonjwa wa maralia na sisi tutazifanyia mgawo katika vituo vyote vya afya nchini kupitia Bohari ya Dawa (MSD)," alisema Msasi

Aliongeza kuwa dawa hizo zitagawiwa na MSD kwa haraka ili wananchi wanufaike kwa wakati kwa kuwa mwisho wa matumizi yake ni Novemba mwakani.

"Dawa hizi zina nembo ya kijani, wananchi watapatiwa kwa gharama ya nusu bei. Hata kwenye soko la kawaida tunashauri ukiona zina nembo ya kijani, mteja anapatiwa kwa nusu bei," alisema.

Meneja Msaidizi wa Shughuli za Bandari, Aloni Kyando, alisema dawa hizo ziliingia nchini Machi 6 mwaka jana na baada ya muda, mteja hakujitokeza kufuata taratibu za forodha.

Kyando aliongeza kuwa kasha la dawa hizo lina jumla ya katoni 360 zenye jumla ya kilo 2,170 na thamani yake ni zaidi ya



Meneja Msaidizi shughuli za Bandari ya Dar es Salaam, Aloni Kyando (wa pili kushoto), akikabidhi hati ya mizigo ya dawa za malaria zilizotelekezwa bandarini kwa Mfamasia Mkuu wa Serikali, Daudi Kisasi, juzi, ili zigawiwe kwenye vituo vya afya. **PICHA: JAMES KANDOYA**

# Ahueni makali mgawo maji yanukia

**Frank Monyo na Julieth Mkireri,** KIBAHA

AHUENI ya mgawo wa maji unaoyakabili baadhi ya maeneo katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani, inanukia baada ya kuwapo taarifa za kuongezeka kwa maji katika Mto Ruvu.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, alisema jana kuwa amepokea taarifa kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kuwa wamewasha mtambo wa kuzalisha maji wa Ruvu Chini baada ya maji kuongezeka Mto Ruvu. Vilevile, Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu imethibitisha kuwa kina cha maji jana kiliongezeka kutoka mita 0.2 mpaka 0.61.

Kunenge alibainisha hayo alipotembelea shamba la raia wa China aliyekamatwa na bonde hilo kwa kosa la kuvuta maji kutoka Mto Ruvu bila kibali.

Alisema agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kwa Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu kufuatilia sehemu ambazo zimechepushwa maji na kuyaruhusu kuingia mtoni, limezaa matunda.

"Ninapenda kuwapongeza Bodi ya Maji Bonde la Wami Ruvu kwa kufanya doria ambayo imezaa matunda kwani nimepokea taarifa kutoka DAWASA kuwa maji yameongezeka mtoni na kupelekea kuwashwa mtambo wa kuzalisha maji wa Ruvu Chini na pia bodi imethibitisha maji kuongezeka kutoka mita 0.2 mpaka 0.61 kwa leo (jana) mchana," alisema.

Kunenge aliagiza kusitishwa shughuli za kilimo cha umwagiliaji kwa wakulima waliokuwa wanatumia maji ya Mto Ruvu.

Alisema ni marufuku kwa mtu yeyote kuendelea kutumia maji ya Mto Ruvu kwa shughuli za umwagiliaji na mifugo hadi pale serikali itakapotoa taarifa nyingine.

Kiongozi huyo aliyekuwa ameongozana na kamati ya ulizi na usalama ya mkoa, Wilaya ya Bagamoyo na Kibaha, alishuhudia baadhi ya wakulima wakiendelea na shughuli za kilimo.

"Wakulima wote wenye vibali vya kutumia maji kwenye Mto Ruvu wasitishe shughuli zao hadi pale yatakapotoka maelekezo mengine, wanaonywesha mifugo na kutumia mashine pia waache mara moja kwani kuendelea kufanya hivyo ni kuhatarisha maisha ya wananchi," aliagiza.

Aliwaonya wanaoiba maji nyakati za usiku na kufanya shughuli za umwagiliaji, akiwataka kuacha mara moja na wakikaidi hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Kunenge aliwaagiza wakurugenzi kuwafuatilia watendaji ambao wanashindwa kuwajibika kwenye maeneo yao na kuwachukulia hatua za kinidhamu.

Alitoa agizo hilo baada ya kubaini uwapo wa wakulima wa umwagiliaji ambao baadhi yao hawajafuata sheria huku mamlaka zinazohusika zikiwa hazina taarifa sahihi za uwapo wao.


**MAJEMBE AUCTION MART LIMITED**
**(VIJANA WA KAZI)**

**NOTISI/MNADA:**

KWA NIABA YA **DIAMOND TRUST BANK P.O BOX 115 DAR ES SALAAM ,** TUNATOA NOTISI KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI KWA WADAIWA WALIYOTAJWA HAPA CHINI WALIPE MADENI YAO WANAYODAIWA KWA MUDA MREFU.
ENDAPO WATASHINDWA KULIPA KWA MUDA ULIOTOLEWA, DHAMANA ZAO ZITAUZWA KWA MNADA WA HADHARA KWA RATIBA IFUATAYO:-

| NA. | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | DHAMANA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1 | MIPA COMPANY TANZANIA LTD | 1)PLOT NO.417 & 418 BLOCK"A" NYAMUHONGOLO AREA MWANZA, 2)NYUMBA ILIYOPO PLOT NO.100 & 81 BLOCK"M" RUFIJII AREA MWANZA CITY, 3) PLOT NO. 1506 BLOCK A. BUSWERU AREA MWANZA CITY. | 27/11/2021;SIKU YA JUMAMOSI KUANZIA SAA NNE ASUBUHI |
| 2 | MWAJI GROUP WORKSHOP LTD/ALLAN MWAIGAGA | NYUMBA ILIYOPO PLOT NO.19 BLOCK "Y" UYOLE AREA, MBEYA CITY. | 04/12/2021;SIKU YA JUMAMOSI KUANZIA SAA NNE ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA:**
A). UKAGUZI UNARUHUSIWA KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI.
B). MALIPO NI 25% YA BEI ITAKAYOFIKIA KWENYE MNADA NA SALIO LITALIPWA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE (14) TU.
C). ENDAPO MNUNUZI ATASHINDWA KULIPA SALIO KWA MUDA ULIOTOLEWA, ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI ZAKE ZOTE NA NYUMBA ITAUZWA TENA

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NASI KWA SIMU NA. MAKAO MAKUU (0784301930, 0745707008), MWANZA (0755244442), MBEYA (0753687242).**


# Samia: Naona fahari, napata ari, ujasiri kuniunga mkono

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema anaona fahari jinsi Watanzania wanavyomuunga mkono katika uongozi wake, hatua ambayo inampa ari na ujasiri mkubwa wa kisiasa.

Alitoa kauli hiyo jana mjini Zanzibar alipohutubia mkutano wa hadhara uliotayarishwa na Umoja wa Wanawake (UWT) kwa ajili ya kumpongeza kufuatia mafanikio ya majukumu yake.

Alisema asili yake ni tunda linalotokana na malezi mazuri kutoka kwa viongozi wake ambao amepitia kwa nyakati tofauti, akimtaja Rais mstaafu Amani Abeid Karume kuwa ndiye aliyemfungulia mwanga wa kisiasa.

"Malezi niliyoyapata ni mazuri kwa walezi wangu na ndiyo maana ni sehemu ya mafanikio yangu ya safari za kisiasa ambapo Rais mstaafu Karume alifunguwa maisha yangu ya kisiasa," alisifu.

Alisema ataendelea kuongoza nchi kwa kufuata misingi ya katiba na sheria ili kuimarisha utawala bora na kuwawezesha wananchi kupata mafanikio makubwa ya kiuchumi na kufaidika na fursa za maendeleo.

Rais Samia alisema katika kipindi kifupi cha uongozi wake, Tanzania imepata mafanikio makubwa katika nyanja mbalimbali ikiwamo kimataifa ambapo diplomasia ya Tanzania nje ya nchi imeimarika.

Alisema kuimarika kwa siasa za nje kumeyafanya mataifa mbalimbali kuishika mkono Tanzania kwa kuiunga mkono katika harakati zake za kuimarisha uchumi na maendeleo.

Rais Samia alisema katika uongozi wake atahakikisha Tanzania inayafikiya malengo ya maendeleo endelevu yaliyowekwa na Umoja wa Mataifa (UN) husu akisisitiza mwanamke hataachwa nyuma katika safari hiyo.

Alisema atahakikisha wanawake wananufaika na fursa mbalimbali zinazopatikana kwa ajili ya kuleta mabadiliko makubwa ya maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii.

Rais Samia pia alisema amerithishwa na uongozi wa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi ambaye ametimiza mwaka mmoja madarakani, akifanikisha mambo ya msingi aliyoyaahidi ikiwamo kupambana na rushwa na kuongeza kasi ya uwajibikaji serikalini.

Alisema katika kipindi chake amefanya kazi kubwa kuongeza kasi ya uwajibikaji huku akionyesha njia na dalili kwamba Tanzania bila rushwa inawezekana.

Rais Samia alisema Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni mfano wa kuleta umoja na utulivu ambao umewaunganisha wananchi wote na kuondosha siasa za chuki na uhasama.

Aliwataka Wazanzibar kuilinda serikali hiyo inayotokana na maridhiano ya kisiasa yaliyofikiwa ambayo yamefungua milango ya baraka ya kuelewana na kuondokana na siasa za chuki na mivutano.

# HABARI KITAIFA

## Moto wateketeza hoteli nne, watalii waokolewa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

BAADHI ya watalii wamenusurika kifo baada ya hoteli walizofikia huko Jambiani, Mkoa wa Kusini Unguja kuteketea kwa moto uliozuka juzi majira saa 11:00 jioni.

Moto huo umeteketeza hoteli nne ambapo tatu kati ya hizo, hakuna kilichotolewa zaidi ya watalii waliokuwamo.

Akizungumza na Nipashe jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kusini Unguja, Suleiman Hassan, alisema moto huo ulianza kuteketeza hoteli ya Villa de Coco kisha kuzifikia hoteli zingine zilizoko karibu.

Alizitaja hoteli hizo ni Spice Island ambayo imeungua vyumba sita vya kulala wageni, Fun Beach na Cobe ambazo zimeteketea zote.

Kamanda Hassan alisema chanzo cha moto huyo bado hakijajulikana, lakini taarifa za awali zinadaiwa kuwa ni hitilafu ya jiko katika hoteli ya Villa de Coco.

Alisema katika ajali hiyo ya moto hakuna kifo wala majeruhi kwa sababu watalii waliokuwapo katika hoteli hizo, waliokolewa haraka na kuhifadhiwa katika hoteli ya Shaharzade.

"Tunashukuru kuwa hakuna kifo wala majeruhi wa moto huu, watalii wote pamoja na wafanykazi wa hoteli hizi waliwahi kutoka. Bado thamani ya gharama ya vitu vilivyoteketea katika hoteli hizi haijajulikana," alisema.

Alifafanua kuwa moto huo ulikuwa mkubwa kutokana na paa la hoteli kuezekwa kwa makuti, lakini ulidhibitiwa majira ya saa mbili usiku juzi.

Kamanda Hassan alisema kila hoteli ina mmiliki tofauti, wote wakiwa ni rai wa kigeni na hana uhakika kama hoteli hizo zimekatiwa bima.

Baadhi ya mashuhuda waliokuwapo katika ajali hiyo, walisema kuwa moto huo haukudhibitiwa mapema na ndio sababu ukasambaa na kuteketeza hoteli zingine.

## CCM yataka uwekezaji zaidi Bandari ya Kigoma

**Na Beatrice Shayo,** KIGOMA



KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka (pichani) amesema kuna haja kuongezwa nguvu katika uwekezaji wa Bandari ya Kigoma ili kuwezesha wananchi kupata huduma.

Shaka aliyasema hayo juzi alipozuru bandarini huko na kubainisha kuwa bado wananchi hawajanufaika na bandari hiyo katika kujikwamua kiuchumi.

Alisema miradi ya ujenzi na ukarabati wa bandari ni utekelezaji wa ibara ya 59 ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM inayoitaka serikali kuimarisha miundombinu ya mawasiliano ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora.

"Kama wanatuambia meli zinazokuja hapa ni za majirani na sisi hatuna meli hata moja ambayo inatoa huduma, hili ni jambo la kuangalia.

"Tena tuliangalie kwa umakini kinachoingia tukiwa na meli zetu na kile cha majirani ni vitu viwili tofauti," alisema.

Shaka pia alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa dhamira yake ya kufungua uchumi wa Kigoma na mikoa jirani.

Alisema wameona ukarabati wa meli mbili ambazo zitabeba abiria 600 na nyingine ya kubeba mafuta.

Shaka alisema kukamilika kwa mradi huo ni kufungua rasmi uchumi wa Mkoa wa Kigoma na kutakuwapo mzunguko wa fedha.

"Rais amekwenda kufungua uchumi wa Kigoma na Kanda ya Ziwa kupitia bandari hii sasa inakwenda kufaidisha wananchi. Waendelee kujipanga vizuri na wawe tayari kutoa huduma.

"Meli ya MV Liemba nadhani tutatoa rai kwa serikali waangalie vizuri maana ni tegemeo la wananchi wa Kigoma kwa kuwa imedumu kwa miaka 108 na bado inaonyesha inahimili kutoa huduma, nadhani ni kuifanyia maboresho wakati huu," alisema Shaka.

Alisema meli hiyo itabaki kuwa kielelezo cha historia kwa sababu wanakwenda kwenye maadhimisho ya miaka 60 ya Uhuru wakiwa na meli hiyo kongwe nchini.

"Tutaithamini kama sehemu ya kukuza utalii wetu na itumike kama kielelezo cha kunyanyua uchumi wetu maana mbunge ameeleza kitu ambacho wanakipenda ni meli hiyo, hawataraji kutokutoa huduma kwa MV Liemba, ni kupotea kwa historia ya Kigoma katika uwekezaji huo wa bandari hasa katika Ziwa Tanganyika," alisema.


### MEM AUCTIONEERS AND GENERAL BROKERS LTD

**HEAD OFFICE: P.O.BOX 32830 DAR ES SALAAM, BRANCH OFFICE: P.O. BOX 76 HIMO MOSHI**

### TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na kiwanda cha sukari **(TPC LTD);** Tutauza kwa mnada wa hadhara magari, matrekta na vitu mbalimbali kama ilivyooredheshwa hapo chini. Mnada utafanyika tarehe 08/12/2021 kuanzia saa 4.00 asubuhi Kiwandani TPC LTD, Moshi, Kilimanjaro. Mali zitakazouzwa ni kama ifuatavyo;

| LOT NO. | AINA YA MASHINE | TPC NA. | TOLEO | MWAKA WA MATENGENEZO | NAMBA YA USAJILI | USHURU WA FORODHA | PUNGUZO KWA WAAJIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | FORD PICK-UP SINGLE CAB | ML150 | RANGER | 2016 | T789DLD | PAID | YES |
| 2 | FORD PICK-UP SINGLE CAB | ML134 | RANGER | 2015 | T928DFH | PAID | YES |
| 3 | FORD PICK-UP SINGLE CAB | ML124 | RANGER | 2014 | T221BDB | PAID | YES |
| 4 | FORD PICK-UP SINGLE CAB | ML123 | RANGER | 2014 | T201DBD | PAID | YES |
| 5 | FORD PICK-UP SINGLE CAB | ML135 | RANGER | 2015 | T268DGC | PAID | YES |
| 6 | FORD PICK-UP SINGLE CAB | ML117 | RANGER | 2014 | T900CTE | PAID | YES |
| 7 | BELL TRACTOR | MF60 | BELL | 2001 | T667AAT | PAID | YES |
| 8 | BELL TRACTOR | MF61 | BELL | 2001 | T944AAT | PAID | YES |
| 9 | BELL GRADER | MG9 | BELL770D | 2005 | T840ANZ | EXEMPTED | NO |
| 10 | BELL FRONT LOADER | ME6 | LOGGER | 2004 | T696ASQ | EXEMPTED | NO |
| 11 | KOMATSU FRONT END | ME6ME14 | WA380-3A | 2007 | T270ASW | PAID | NO |
| 12 | BACK HOE LOADER | ME18 | LOADER 580M | 2012 | T383CRH | PAID | NO |
| 13 | BELL GRADER | MG11 | 770G | 2011 | T519BSS | PAID | NO |
| 14 | KOMATSU FRONT END | MG15 | WA380-3 | 2009 | T436BLT | EXEMPTED | NO |
| 15 | LORRY NISSAN DIESEL | MR20 | UD | 2010 | T722CAY | PAID | NO |
| 16 | RENAULT TIPPER LORRY | MR15 | VE6 | 2008 | T560BDW | PAID | NO |
| 17 | RENAULT TIPPER LORRY | MR16 | VE6 | 2008 | T541BDW | PAID | NO |
| 18 | LEYLAND ASHOK | MR17 | 912 | 2007 | T152BES | PAID | NO |
| 19 | TOYOTA COASTER | MR89 | 1HZ | 2010 | T936BNP | PAID | NO |
| 20 | NISSAN UD DIESEL BOWSER | MR19 | UD | 2011 | T914BYH | PAID | NO |
| 21 | SLASHER | MP64 | POWA | N/A | N/A | N/A | YES |
| 22 | FERTILIZER APPLICATER | MP60 | REAPER | N/A | N/A | N/A | YES |
| 23 | FERTILIZER APPLICATER | MP49 | REAPER | N/A | N/A | N/A | YES |
| 24 | BOOM SPRAYER | MP74 | BERTHOUD | N/A | N/A | N/A | YES |
| 25 | CONCREATE MIXER | MU69 | | N/A | N/A | N/A | NO |
| 26 | CONCREATE MIXER | MU68 | | N/A | N/A | N/A | NO |
| 27 | BOOM SPRAYER | MP105 | BERTHOUD | N/A | N/A | N/A | NO |
| 28 | KUHN SLASHER | MP75 | BPR305 PRO | N/A | N/A | N/A | NO |
| 29 | MUD TRAILLER | MP60 | DEVES | N/A | N/A | N/A | NO |
| 30 | HONDA WATER PUMP | MU2 | HONDA | N/A | N/A | N/A | YES |
| 31 | KUDU ROTARY SLASHER | MU46 | 750 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 32 | KUHN MUTLILONGER SLASHER | MP93 | KUNH | N/A | N/A | N/A | NO |
| 33 | SLASHER | MP45 | SLASHER | N/A | N/A | N/A | NO |
| 34 | LAWN MOWER SLASHER | MP44 | MASTER | N/A | N/A | N/A | YES |
| 35 | GENERATOR | GEN124 | HONDA GX270 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 36 | GENERATOR | MU101 | HONDA GX270 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 37 | GENERATOR | GEN102 | HONDA GX270 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 38 | GENERATOR | GEN81 | HONDA GX270 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 39 | GENERATOR | GEN118 | HONDA GX270 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 40 | GENERATOR | GEN103 | HONDA GX270 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 41 | KUDU ENGINE | MU80 | HONDA GX390 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 42 | GENERATOR | N/A | HONDA GX270 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 43 | HONDA GENERATOR | N/A | HONDA GX160 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 44 | HONDA WATER PUMP | N/A | HONDA GX160 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 45 | HONDA WATER PUMP | N/A | HONDA GX160 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 46 | HONDA WATER PUMP | N/A | HONDA GX160 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 47 | CHAIN SAW | MU133 | STIHL MA6610 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 48 | CHAIN SAW | MU134 | STIHL MA6610 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 49 | CHAIN SAW | MU132 | STIHL MA6610 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 50 | CHAIN SAW | MU107 | STIHL MS382 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 51 | CHAIN SAW | MU141 | STIHL MS382 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 52 | CHAIN SAW | MU122 | STIHL MS382 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 53 | RAIL GRINDER | MU109 | GEISMAR | N/A | N/A | N/A | YES |
| 54 | BRUSH CUTTER- | N/A | MARUYAMA | N/A | N/A | N/A | YES |
| 55 | BRUSH CUTTER | MU96 | MARUYAMA | N/A | N/A | N/A | YES |
| 56 | BRUSH CUTTER | MU106 | STIHL FS450 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 57 | LAWN MOWER | MU105 | PROFESSIONAL | N/A | N/A | N/A | YES |
| 58 | LAWN MOWER | MU119 | HONDA196 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 59 | MIST BLOWER | MU04 | WARRIOR | N/A | N/A | N/A | YES |
| 60 | MIST BLOWER | N/A | MARUYAMA MD180DX | N/A | N/A | N/A | YES |
| 61 | MIST BLOWER | N/A | WARRIOR | N/A | N/A | N/A | YES |
| 62 | MIST BLOWER | N/A | WARRIOR | N/A | N/A | N/A | YES |
| 63 | MIST BLOWER | N/A | WARRIOR | N/A | N/A | N/A | YES |
| 64 | MIST BLOWER | N/A | WARRIOR | N/A | N/A | N/A | YES |
| 65 | LOW BED | MT71 | ANGLOCO SPM UK 111A | N/A | N/A | N/A | NO |
| 66 | FERTILIZER APPLICATER | MP6 | SPREADER | N/A | N/A | N/A | YES |
| 67 | PRINTING ACCESSORIES | N/A | | N/A | N/A | N/A | NO |
| 68 | VARIOUS PARTS FOR BOOM SPRAYER | N/A | | N/A | N/A | N/A | NO |
| 69 | VARIOUS PARTS FOR KOMATSU FRONT END LOADER | N/A | | N/A | N/A | N/A | NO |
| 70 | VARIOUS PARTS FOR KUHN SLASHER | N/A | | N/A | N/A | N/A | NO |
| 71 | VARIOUS PARTS FOR CAT& GRADER | N/A | | N/A | N/A | N/A | NO |
| 72 | VARIOUS PARTS FOR ISUZU CVR | N/A | | N/A | N/A | N/A | NO |
| 73 | VARIOUS PARTS FOR MITSUBISH CANTER | N/A | | N/A | N/A | N/A | NO |
| 74 | BRONZE &TILES | N/A | | N/A | N/A | N/A | NO |
| 75 | VARIOUS GASKET KITS,RINGS, "O"RINGS & SEALS | N/A | | N/A | N/A | N/A | NO |
| 76 | KEMGUARD&DISPENSERS | N/A | | N/A | N/A | N/A | NO |
| 77 | VARIOUS SIZES OF WINDOW FRAMES | N/A | | N/A | N/A | N/A | NO |
| 78 | VARIOUS SIZES OF WINDOW FRAMES | N/A | | N/A | N/A | N/A | NO |
| 79 | WATER STORAGE TANK 10,000 LTS | N/A | SIM TANK | N/A | N/A | N/A | NO |
| 80 | WATER STORAGE TANK 5,000 LTS | N/A | SIM TANK | N/A | N/A | N/A | NO |

**MASHARTI YA MNADA:**

1. Mali zitauzwa kama zilivyo.
2. Mnunuzi atalazimika kulipa fedha taslimu ya 25% mara tu baada ya nyundo ya dalali kutua na salio la 75% kulipwa ndani ya saa 48.
3. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti namba mbili hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mali itauzwa kwa mshindi wa pili.
4. Ukaguzi wa mali utafanyika tarehe 06/12/2021 na 07/12/2021 kuanzia saa Tatu asubuhi mpaka saa kumi jioni.
5. Mnunuzi atatakiwa kuondosha mali katika eneo la mnada mara tu baada ya kukamilisha taratibu za malipo na kodi za serikali.
6. Mali zote zitakazouzwa chini ya milioni moja zitatakiwa kulipiwa kikamilifu siku hiyo hiyo na kuondolewa eneo la mnada.
7. Kwa maelezo zaidi wasiliana na **Dalali kwa Na. 0713/0754 262 400, 0756 606 671**

216581102

RIPOTI MAALUM -2

# Mwanadada 'alivyotoka' kupitia kilimo mseto

## ■Utafiti wa TARI wabaini faida maradufu
## ■Wizara yahimiza fursa ichangamkiwe

**Na Mwandishi Wetu,** KOROGWE

**KATIKA toleo la kwanza la ripoti hii wiki iliyopita, ilielezwa kwa kina namna kijana Monica Mizambwa, mkulima mdogo wa mkonge wilayani Korogwe mkoani Tanga, alivyoupiga teke umasikini baada ya kujikita kwenye kilimo mseto, akilima mahindi, maharagwe na mimea jamii ya kunde kwenye shamba lake la mkonge.**

**Leo kwenye shehemu ya mwisho ya ripoti kuna ufafanuzi wa kina kutoka kwa wataalamu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) na serikali kuhusu kilimo mseto, hususan kwa wakulima wadogo wa mkonge. Endelea...**

**UTAFITI WA TARI**

Peter Mbilinyi, Ofisa Utafiti wa TARI Kituo cha Mlingano mkoani Tanga, anasema utafiti wao kuhusu kilimo mseto cha mkonge na mazao mengine katika mikoa ya mashariki mwa Tanzania, umebaini ubunifu huo umekuwa na tija kwa wakulima.

Mbilinyi anasema utafiti wao huo walioufanya kuanzia mwaka 2012 na matokeo yake kuwasilishwa mwezi uliopita kwa wafadhili wao, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), umebaini uchanganyaji mazao kwenye mashamba ya mkonge umekuwa na matokeo chanya kwa wakulima wadogo wilayani Korogwe na Muheza mkoani Tanga.

Anasema tija imeonekana kwenye mashamba yaliyoko Mwelya, Ngombezi, Magoma, Magunga, Kibaranga, Hale na Ngombezi, mafanikio kama hayo yakiripotiwa pia kutoka kwa wakulima wengine wa mkonge eneo la Kihonda mkoani Morogoro na mikoa ya Kanda ya Ziwa, hususan Shinyanga na Mara.

Kama ilivyofafanuliwa na Ofisa Kilimo Monica, mtafiti huyo wa TARI pia anaunga mkono hoja kwamba mseto wa mkonge na mimea jamii ya kunde husaidia urutubishaji wa udongo kutokana na mimea hiyo kuwa na kiwango kikubwa cha naitrojeni.

Anasema kituo chao (TARI Mlingano) tayari kimetoa elimu na kusambaza ubunifu huo kwa wakulima wadogo wapatao 100.

"Utafiti wetu umebaini kilimo cha mkonge na mseto wake kinapunguza gharama za palizi kwa asilimia 50. Mseto wa mkonge, mahindi na jamii ya mikunde unamwongezea mkulima usalama wa chakula na kipato.

"Tumebaini mseto huo unatoa wastani wa Kg 700 hadi 1,500 za mahindi kwa hekta na Kg 1,000 hadi 2,200 za kunde kwa hekta," anabainisha.



Waziri wa Kilimo, Prof Adolf Mkenda.

Tafsiri ya kiwango hicho ni sawa na wastani wa maguni saba hadi 15 ya mahindi kwa hekta na wastani wa magunia 10 hadi 22 ya kunde kwa hekta.

Mtafiti Mbilinyi anapendekeza kuwa kwa manufaa ya nchi, elimu ya kilimo cha mkonge na mseto wake ifikishwe kwa wakulima wadogo wengi zaidi nchini.

**RAI YA WAZIRI**

Waziri wa Kilimo, Profesa Adolf Mkenda, anaunga mkono hoja hiyo, akisema tayari wataalamu wa wizara hiyo wanahamasisha Watanzania kulima mkonge na kuutumia ubunifu wa TARI wa kuchanganya mazao mengine kwenye mkonge ambao haujakomaa.

Prof. Mkenda anabainisha kuwa hadi Aprili mwaka huu, TARI kwa kushirikiana na wadau wa kilimo imezalisha na kusambaza miche milioni 13.56 ya mazao ya viazi vitamu, zabibu, minazi, parachichi, miwa, mkonge na pingili za muhogo milioni 40.9.

Waziri huyo anafafanua zaidi kuwa kwa mwaka 2020/21, uzalishaji wa mazao asilia ya biashara ya tumbaku, pamba, kahawa, chai, pareto, korosho, mkonge na sukari ulifikia tani 876,510.83.

"Katika mwaka 2020, mchango wa kilimo katika Pato la Taifa (GDP) ulikuwa ni asilimia 26.9. Katika kipindi hicho, sekta ya kilimo imekua kwa asilimia 4.9 kulinganishwa na asilimia 4.4 ya mwaka 2019.

"Pia katika mwaka 2020, sekta ya kilimo ilichangia kwa asilimia 58.1 katika kutoa ajira nchini na kuchangia zaidi ya asilimia 65 ya malighafi za viwanda nchini," anasema.

Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Kimataifa la Usimamizi wa Kilimo Misitu (ICRAF), Dk. Anthon KImaro, anasema asilimia 32 ya wakulima nchini wameshajiingiza kwenye kilimo mseto na wanapata manufaa ya kulima mazao mchanganyiko.

**MIKAKATI SERIKALINI**

Januari 20 mwaka huu, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akiwa Kituo cha TARI Mlingano wilayani Muheza mkoani Tanga, aliziagiza halmashauri zote zinazolima mkonge kuanzisha vitalu vya kuzalisha miche bora ya mkonge na kuigawa kwa wakulima ili kufufua mashamba zaidi na kuongeza uzalishaji zao la mkonge nchini.

Majaliwa pia aliutangaza mkonge kuwa miongoni mwa mazao ya kimkakati nchini ili kuinua uchumi wa nchi na kutatua tatizo la uhaba wa ajira kwa vijana linalotikisa nchini kwa sasa.

Siku hiyo, Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema wizara yake imejipanga kuhakikisha mikoa mingi zaidi inalima mkonge ili kuongeza uzalishaji toka tani 36,298 za sasa hadi tani 120,000 ifikapo mwaka 2025.

Bashe alisema ili kuongeza kasi ya uzalishaji na ufufuaji mashamba ya mkonge nchini, wizara imepanga kuzuia uagizaji magunia nje ya nchi kwa bodi za mazao zote kutakiwa kutumia magunia ya katani yanayozalishwa nchini.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Mkonge Tanzania, Saad Kambona, mkonge sasa unalimwa katika mikoa 18 nchini, lakini hulimwa zaidi katika mikoa ya Tanga, Morogoro, Arusha, Mwanza, Shinyanga na Kilimanjaro.

**USULI NA HISTORIA**

Kwa mujibu wa TARI Mlingano, historia ya kilimo cha mkonge Tanzania inaanzia mwaka 1892 pale mtaalamu wa Kijerumani, Dk. Richard Hindorff, mtafiti wa mimea na udongo, alipouingiza nchini.

TARI Mlingano wanarejea historia hiyo, wakisema mtaalamu huyo alichukua miche 1,000 kutoka pwani ya Mexico kwenye Jimbo la Yuctan ambalo ndiyo asili ya jina 'katani' na kuisafisha kwa magendo kupitia Frolida, Marekani na Humburg, Ujerumani.

"Kati ya miche 1,000, ni miche 62 tu ndiyo iliyofika Tanganyika na ilipandwa sehemu iitwayo Kikokwe huko Pangani ,Tanga.

"Mkonge ulisambaa maeneo mengi ya Tanganyika. Hadi kufikia mwanzoni mwa miaka 1960, Tanganyika ilikuwa inaongoza kwa uzalishaji wa mkonge ikifuatwa na Brazil na Mexico kwa mauzo ya tani 230,000 kwa mwaka nje ya nchi.

"Kutokana na sababu mbalimbali zilizojitokeza miaka ya 1970, uzalishaji ulipungua toka tani 230,000 hadi tani 19,700 kwa mwaka 1997.

"Hata ivyo mageuzi ya kiuchumi yaliyoanza miaka 1980 ambayo yalilenga katika ubinafsishaji na biashara huria, uhuru wa taasisi za kifedha za ndani na nje ya nchi, vyote vikafufua kilimo cha mkonge na hasa kukamilika kwa ubinafishaji mwaka 2005, uzalishaji ulipopanda hadi kufikia tani 40,000 mwaka 2015," inabainishwa na kituo hicho cha utafiti.

Kwa mujibu wa kituo hicho, soko kuu la mkonge wa Tanzania ni China, Saudi Arabia, India, Hispania, Ujerumani, Uingereza, Kenya, Uganda na Nigeria.



Monica akifurahia mafanikio ya kazi yake.



Uvunaji wa mkonge ukiendelea kwenye shamba la Monica.

RIPOTI MAALUM

# Mapenzi yanavyochochea kasi ongezeko la magonjwa ya akili

**Na Renatha Msungu,** DODOMA



SITAKI kabisa kusikia mwanamke wa Kiafrika kutokana na kilichonikuta hadi nikawa na matatizo ya afya ya akili," Felix Mwinuka anasimulia mkasa na chanzo cha kuwa miongoni mwa wateja wa Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe mkoani Dodoma.

Mwinuka (48), ambaye kwa sasa ni miongoni mwa walimu wa Shule ya Msingi Mbwanga mjini Dodoma, anasimulia kuwa akiwa wilayani Kongwa Machi 1992, alipata shida kwenye afya ya akili baada ya kusalitiwa na aliyekuwa mchumba wake.

Akizungumza kwa hisia na kujutia uamuzi wake anaoutaja wa kupenda kupitiliza,

Mwalimu Mwinuka anasimulia kilichojiri, akitamka:

"Kwa kweli nilimpenda sana ... (anataja jina la aliyekuwa mchumba wake), Tuliwekeana ahadi ya kuoana tangu tukiwa kidato cha pili, lakini tulipohitimu haikuwa hivyo kwani mimi niliishia Mirembe kupatiwa matibabu, yeye akawa na mwanamume mwingine.

"Kilichotokea hadi nikalazimika kupelekwa Mirembe ni taarifa nilizopata kwamba mchumba wangu anatembea na bwana mwingine. Iliniuma sana kwa sababu nilikuwa nimemzoea sana.

"Niliamua kwenda alikokuwa anaishi kule Kongwa. Nilimkuta anasikiliza muziki, nikaungana naye lakini baada ya dakika chache aliingia yule mwanamume aliyekuwa anatembea naye.

"Uliibuka ugomvi mkubwa pale, nikapigwa na yule mwanamume mbele ya mchumba wangu. Kwa kweli alinidhalilisha sana. Uamuzi wangu wa awali ulikuwa kujiua tu, nisionekane tena kwenye eneo hilo, lakini haikuwa hivyo."

Mwalimu Mwinuka anaendelea kusimulia kilichojiri kwamba baada ya kipigo hicho, alisafiri umbali mrefu kwa baiskeli kutoka kijiji alikokuwa anaishi mchumba wake huyo pasi na kujua alikokuwa anakwenda.

"Baadaye nilishtuka, nikajiuliza 'ninakwenda wapi?' Ndipo nikaamua kurejea nyumbani, lakini nilizidi kuchanganyikiwa kutokana na fedheha iliyonipata.

"Nikiwa pale nyumbani, familia ilibaini nimepata tatizo la akili, ikaamua kunipelekea Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili (Mirembe) ili kupatiwa matibabu," anasimulia.

Mwalimu Mwinuka anasema matibabu hayo yalichukua takriban mwezi mmoja, akapona na kuendelea na majukumu yake ya ujenzi wa taifa.

"Wakati ninapata hilo tatizo nilikuwa mwanafunzi wa kidato cha tano pale Mazengo. Nilipopona sikurejea tena shuleni, ilibidi nitumie cheti changu cha kidato cha nne kuchukua kozi ya ualimu wa shule za msingi.

"Kwa sasa mimi ni mwalimu na tangu kipindi hicho sijawahi kufikiria kuoa mwanamke wa Kiafrika. Ninatarajia kuoa mzungu, ninaamini nitaishi naye vizuri bila bugudha.

"Muda mwingi ninapokuwa nje ya majukumu ya ualimu, ninasoma vitabu na ninaandika vitabu vyangu pia. Hii imenisaidia kuepuka kufikiria mambo ya mapenzi ambayo yalinipa shida sana," Mwalimu Mwinuka anahitimisha.

**WATAALAMU MIREMBE**

Dk. Godwin Mwisonge, anayeshughulikia masuala ya akili katika Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe, anaeleza uzoefu wake kwamba watu wengi wanapata ugonjwa wa afya ya akili kutokana na kushindwa kuhimili matukio yanayotokea dhidi yao.

Anabainisha kuwa kuna magonjwa ya afya ya akili zaidi ya 300 na kila mtu anaweza kupata tatizo hilo kulingana na mazingira anayoishi.

"Ziko kesi nyingi sana za masuala ya afya ya akili zinazosababishwa na uhusiano wa kimapenzi, lakini utafiti wa kisayansi bado haujafanyika kubaini ni kwa kiasi gani hapa Mirembe tuna wagonjwa wa aina hiyo ambao kiini ni mapenzi.

"Kesi zipo na huwa zinawachukua muda kupona, wengine hupona baada ya wiki tatu na kurejea mtaani, wengine huchukua muda zaidi kupona, lakini kesi nyingi za aina hiyo huwa tunazitatua hapa ndani ya wiki tatu," anasema.

Mtaalamu huyo anabainisha kuwa kinachorahisisha matibabu hayo ni matumizi ya mfumo maalum wa kutambua suala hilo na matibabu kufanyika haraka.

"Unampokea mgonjwa ana mawazo ya kwamba wameachwa, wamepotezewa muda au kudhalilishwa. Mgonjwa akishikilia msimamo huo kwamba inamuuma kwa sababu hizo, inamchukua muda kweli kupona maana anakuwa kashikilia masuala yake yaliyopita badala ya kuangalia mbele.

"Ikifika hapo sasa inategemea na akili ya mtu ikoje katika kupokea changamoto hizo ambazo anakumbana nazo ili kujikwamua kutoka kwenye matatizo ya akili," anafafanua.

Dk. Mwisonge anabainisha kuwa ingawa utafiti wa kisayansi bado haujafanyika kubaini vyanzo vikuu vya matatizo ya afya ya akili kwa wateja wanaopokewa Mirembe, uzoefu wake unaonyesha wagonjwa wengi wanaofikishwa hospitalini huko wamepata tatizo kutokana na mapenzi.

"Matibabu yanategemea na wewe mwenyewe ulivyolipokea tatizo hilo, ukifikishwa hospitalini bado una fikra za 'kwa nini kaniacha na kunipotea muda?' inatuwia ugumu sana kukutibu na kukuponesha haraka kwa sababu tunakutibu ilhali bado unawaza ya nyuma," anasema.

Katika kukabiliana na tatizo la afya ya akili nchini, Dk. Mwisonge anabainisha mikakati yao kwamba inajumuisha kutoa elimu kwa jamii kuhusu masuala ya afya ya akili.

"Elimu kuhusu afya ya akili bado haijapewa kipaumbele kwa jamii. Elimu hii ni muhimu kwa jamii kujenga ustahimilivu pale kunapotokea dosari katika uhusiano wa kila siku.

"Lazima jamii itambue kwamba ubongo unapokea vitu vingi, hivyo isikubali kamwe kuuchosha ubongo kwa masuala ya kuharibika kwa uhusiano wa kimapenzi," anashauri.

Paschal Thomas, mkazi wa Dodoma mjini, anasema ameshuhudia baadhi ya watu wakipata ugonjwa wa afya ya akili kutokana na mapenzi na wanapona baada ya kupatiwa matibabu na ushauri wa madaktari.

**KUTOKA WIZARANI**

Dk. James Kihorogwe, Mkurugenzi Msaidizi wa Kitengo cha Magonjwa Yasiyoambukiza wa Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, anasema kuwa mbali na mapenzi, vyanzo vingine vya ugonjwa wa afya ya akili ni pamoja na matumizi ya dawa za kulevya na msongo wa mawazo.

"Jamii inapaswa kuwatunza na kusaidia wagonjwa wa afya ya akili ikiwa ni pamoja na kuwafikisha hospitalini haraka.

"Hakuna sababu ya kuwanyanyapaa watu wenye tatizo la afya ya akili kwa sababu linatibika na linaweza kumpata mtu yeyote yule kulingana na atakavyopokea tatizo lililompata, likiwamo hilo la kuachwa katika uhusiano wa kimapenzi," anasema.

Mkurugenzi huyo anasema Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe ipo kwa ajili ya kuwatibu wagonjwa wenye tatizo la afya ya akili ya aina mbalimbali.

**HALI ILIVYO KITAIFA**

Oktoba 10, mwaka huu, Wizara ya Afya kupitia Kurugenzi ya Magonjwa Yasiyoambukiza, ilibainisha kuwa takriban watu milioni saba nchini wanakadiriwa kuwa na tatizo la afya ya akili, huku Mkoa wa Dar es Salaam ukitajwa kuwa kinara.

Takwimu linganishi ni sawa na asilimia 11.8 ya Watanzania wote wanaokadiriwa kuwa milioni 59 mwaka huu, wanakabiliwa na ugonjwa huo.

Takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) zinaonyesha hadi kufikia mwaka jana (2020), watu bilioni moja duniani walikuwa wanaishi na magonjwa ya akili huku wengi walio katika hatari ni wenye umri kuanzia miaka 15 hadi 39.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Magonjwa ya Afya ya Akili ya Mirembe, Dk. Paul Lawala, alikaririwa siku hiyo akisema ugonjwa wa afya ya akili ni tatizo kubwa duniani kwa kuwa takwimu zinaonyesha watu milioni 300 duniani wanakabiliwa na tatizo la afya ya akili na wanahitaji msaada wa kisaikolojia na waliofikia viwango vya juu wanahitaji matibabu.

Alisema Tanzania ina vikwazo viwili katika kuwahudumia wagonjwa hao ambavyo ni uhaba wa hospitali za kuwatibu na mara nyingine hata waliotibiwa wanakabiliwa na kutokubalika kwa jamii inayowazunguka.

Dk. Lawala alibainisha kuwa Hospitali ya Mirembe ina vitanda 590, lakini hadi Oktoba 9, mwaka huu, ilikuwa na wagonjwa wenye matatizo ya afya ya akili wapatao 400.

Meneja wa Mpango wa Taifa wa Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza kutoka Wizara ya Afya, Dk. Omary Ubuguyu, anabainisha kuwa idadi ya wagonjwa wa akili imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka.

"Mwaka 2018 tulikuwa na wagonjwa 357,799 waliokwenda kupatiwa matibabu, 2019 walikuwa 380,000, mwaka 2020 walifika zaidi ya 500,000," Dk. Ubuguyu anafafanua.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uchunguzi ufanyike sakata mkulima kujiunganishia maji

**MAENEO** mbalimbali katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani yanakabiliwa na uhaba wa maji kwa zaidi ya wiki kutokana na kupungua kwa kina cha maji katika Mto Ruvu ambao ndio tegemeo kubwa la huduma hiyo.

Hatua hiyo imesababisha maeneo hayo kuanza kupata maji kwa mgawo kutokana na kiwango kinachozalishwa kutokutosheleza mahitaji ya huduma hiyo.

Kwa mujibu wa wataalamu wa hali ya hewa, ukosefu huo wa maji umetokana na mabadiliko ya tabia ya nchi pamoja na shughuli za kibinadamu zinazofanyika katika vyanzo vya maji.

Katika wiki hii, kwa mfao, maeneo kama Manzese, Mburahati, Tabata, Segerea, Kinyerezi na Ukonga, imeonekana misururu ya watu wakiwa na madumu kusaka maji huku bei ya maji, yasiyo salama kwa afya za watumiaji, yakiuzwa kwa bei ya juu.

Aidha, uhaba huo wa maji, unaweza kusababisha kuibuka kwa magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu, kuhara na kuhara damu na hata kusababisha baadhi ya wananchi kupoteza maisha. Hali hiyo inatokana na ukweli kwamba wananchi watalazimika kunywa maji yasiyo salama kwa afya zao.

Kutokana na hali hiyo, Rais Samia Suluhu Hassan aliagiza kufanyika kwa jitihada za kudhibiti upotevu wa maji ikiwamo kuwasaka na kuwachukulia hatua watu wanaoharibu vyanzo vya maji.

Hata hivyo, zikiwa hazijatimia saa 24 tangu Rais atangaze amri hiyo, mkulima mkubwa, raia wa China, alinaswa kwa madai ya kujiunganishia maji kutoka Mto Ruvu kwa kutumia mashine yenye uwezo wa kuvuta lita milioni moja kwa ajili ya kumwagilia bustani yake ya Mboga katika Kijiji cha Kidogozelo, Chalinze mkoani Pwani.

Taarifa ya maofisa wa Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu ilibainisha kuwa mtu huyo alikamatwa katika doria waliyoifanya Novemba 12, mwaka huu, akiwa anatumia maji hayo bila kibali na kutozwa faini ya Sh. milioni tatu pamoja na kuzuiwa kutumia maji hayo.

"Cha kwanza tulimkagua na kubaini hana kibali cha Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu kutumia maji ya mto. Tulichukua mashine yake na tukamtaka afike ofisini kwa ajili ya kulipa faini. Novemba 15, akifika ofisini na kulipa faini na tukamzuia kuendelea na umwagiliaji.


Licha ya kutumia maji hayo kinyemela, mkulima huyo, raia wa kigeni, anahusika pia kuchafua mazingira kutokana na kutumia mashine hiyo ya dizeli ambayo ameifunga kwenye mto.

Hatua zilizochukuliwa ndani ya muda mfupi juu ya kukamatwa kwa mkulima huyo ni za kupongezwa lakini kuna jambo la kutafakari zaidi ili kupata majibu ni ujasiri gani anaupata mpaka kufikia hatua hiyo? Tunasema hivyo kwa sababu kwa mtazamo wa kina, kuna jambo limejificha juu ya mkulima huyo kuthubutu kufanya kitendo hicho.

Inawezakena wako baadhi ya watumishi wa umma wasio waaminifu ambao wamejificha nyuma ya pazia. Kwa mtazamo yakinifu, haiwezekani raia wa kigeni akafanya kitendo hicho kwenye ardhi ya nchi nyingine tena bila woga.

Kutokana na mtazamo huo, suala hilo lisiishie kumchukulia hatua mkulima huyo badala yake taasisi zilizopewa dhamana ya kuchunguza mambo zilifuatilie jambo hilo. Kuna uwezekano mkubwa ukaguzi ukifanyika, mengi yaliyojificha nyuma ya pazia yataibuka na kupata ukweli na undani wa sakata zima.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Unachuma mboga saa ngapi kulinda virutubisho?

Na Sabato Kasika

**MBOGA** za majani ya kijani kwa ujumla wake, zina virutubisho muhimu kwa mwili wa binadamu, kuanzia vitamini A na C, lakini pia madini chuma ambayo yanahitajika katika utengenezaji wa kemikali katika seli nyekundu.

Kwa kawaida, mboga nyingi hutoka kwenye majani ya mimea ambayo huwa ya rangi ya kijani, na hutengeneza chakula cha mmea kutoka kwenye mionzi ya jua na huwa na virutubisho vingi muhimu katika mwili wa binadamu.

Miongoni mwa mboga hizo ni figiri, matembele, spinachi, mchicha, majani ya maboga, kisamvu na nyingine nyingi za aina hiyo, huitwa mboga za majani ambazo zote zina virutubisho ambavyo ni muhimu kwa binadamu.

Hata hivyo, inaelezwa kuwa baadhi ya watu huamini kwamba, mboga za majani ya kijani ni chakula cha watu maskini, na hudhani hazina hadhi ya kutumiwa na watu wenye uwezo wao kifedha.

Lakini wataalamu wa lishe wanaweka wazi kwamba, mboga zote za majani zina kitu kimoja muhimu kwa ajili ya miili yetu kama vile vitamini nyingi na madini zaidi ya vyakula vingine na zinatakiwa kuliwa na watu wote.

Pamoja na hayo, mboga za majani sio ghali sana, unafuu wake unamfanya kila mtu mwenye uwezo wa kifedha na asiye na uwezo huo kumudu gharama yake ili naye aweze kufaidi virutubisho vilivyo.

Aidha, inaelezwa kuwa kuna makosa kadhaa ambayo hufanyika katika uchumaji, uandaaji hadi upikaji wa mboga hizo, hali ambayo inaweza kusababisha mlaji kukosa virutubisho hivyo vilivyomo ndani ya mboga.

Ni kawaida kukuta mtu akichuma mboga wakati wowote, kuikatakata, kuiosha na kisha kuipika bila kuifunika, hali ambayo inaelezwa ni sawa na kuondoa virutubisho ambavyo mlaji anatakiwa kuvipata kutoka katika mboga.

Utaratibu huo wa uandaaji mboga ambao umezoeleka kwa watu wengi, unapingwa na Ofisa Lishe wa Jiji la Dar es Salaam, Neema Mwakasege ambaye anataka jamii ibadilike iachane na mazoea.

> **Lakini wataalamu wa lishe wanaweka wazi kwamba, mboga zote za majani zina kitu kimoja muhimu kwa ajili ya miili yetu kama vile vitamini nyingi na madini zaidi ya vyakula vingine na zinatakiwa kuliwa na watu wote.**

Katika ufafanuzi wake, ni kwamba mboga za majani zinatakiwa kuchuma saa 12 alfajiri au saa 12 jioni wakati jua limeshaisha nguvu, kwa kuwa linapowaka linaondoa virutubisho kwenye mboga.

Linakuja suala la uandaaji, ni kwamba mboga inatakiwa kuoshwa ndipo ikatwekatwe na siyo kukatwa na kisha ioneswe, kwa kuwa hatua hiyo nayo inaondoa virutubisho ambavyo mlaji anahitaji kuvipata.

Pamoja na hayo anaona ni vizuri mboga hizo zikapikwa bila kukatwakatwa, kwa kuwa kufanya hivyo kuongeza uwezekano wa kupoteza virutubisho muhimu kwa ajili ya afya ya binadamu.

Kwenye suala la kupasha mboga hizo, inashauriwa kuwa ingefaa kama mtu ataepuka kuzipasha mara kwa mara, ili ziendelee kutunza virutubisho vilivyomo, ambavyo mlaji anatakiwa kuvipata.

Haishiii hapo, bali katika ufafanuzi wake, anaweka wazi kuwa hata wakati wa kupika, sufuria inatakiwa kufunikwa ili mvuko usiondoe virutubisho, na pia baada ya kuiva, iachwe kwa muda kidogo kabla ya kufunuliwa.

Kwamba, jamii ikizingatia maelekezo hayo, ulaji wa mboga za majani utakuwa na maana kwa kuwa itapata virutubisho inavyotakiwa kwa ajili ya kuboresha afya badala ya kufanya maandalizi kwa mazoea.

Mboga za majani ni aina ya chakula ambayo ni muhimu katika kuimarisha na kujenga miili yetu, lakini tatizo kubwa ambalo wataalam wa lishe wanaliona ni watu kutozingatia uandaaji wa mboga hizo hadi kupika.

Lakini pia wanagusia jinsi ya utunzaji wake, kwamba ikitokea mtu amenunua mboga, aweke kwenye jokofu la barafu lenye nyuzi 4 au chini ya hapo ili kutunza virutubisho vyake vya muhimu.

Njia nyingine wanayotaja katika kufanikisha hilo, kutunza vyakula kwenye sehemu ya giza na ubaridi, kwa kuwa vyakula vingi hupoteza virutubisho vyake vinapowekwa sehemu za mwanga na joto.

**SAFU**

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Utouh amesema ukweli, bila uwazi hakuna uwajibikaji



Na Pascal Mayalla

**Serikali iliwakilishwa na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, ambaye ndiye alifungua kongamano hilo ambalo lengo lake kuu ni kujenga utawala bora. Mongela amefungua kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba ambaye pia alikuwa akimwakilisha Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango.**

WIKI hii nilikuwa jijini Arusha kuhudhuria kongamano la kimataifa maarufu kama ITAC, kujadili umuhimu wa uwazi na uwajibikaji katika kusukuma mbele maendeleo, si tu kwa Tanzania bali bara lote Afrika. Kongamano hilo liliandaliwa na taasisi isiyo ya kiserikali inayojihusisha na masuala ya uwazi na uwajibikaji ya WAJIBU.

Mkurungenzi Mtendaji wa Taasisi hiyo, Ludovick Utouh, (aliyekuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali- CAG), alisema bila kuwapo uwazi katika utendaji wa serikali, uwajibikaji hautakuwapo. Ili uwajibikaji uwapo, ni lazima kwanza utanguliwe na uwazi na baada ya kuwapo kwa uwazi kwa kila mtu kujua kila kinachofanyika, watendaji watajikuta wanalazimika kuwajibika maana kila kitu kitakuwa wazi.

Utouh aliyasema hayo katika mahojiano na mwandishi wa makala hii wakati akilitambulisha kongamano la kimataifa hilo, kujadili umuhimu wa uwazi na uwajibikaji katika kusukuma mbele maendeleo ya Tanzania na Afrika kwa ujumla.

Alisema kongamano hilo lina umuhimu wa kipekee kwa sababu bila kuwa na uwazi katika utendaji kazi serikalini, utendaji unakuwa haupo na kusisitiza hoja za uhitaji wa serikali kutenda kazi kwa uwazi ni takwa la kikatiba na lipo kwenye Katiba ya Tanzania ya mwaka 1977.

Serikali iliwakilishwa na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, ambaye ndiye alifungua kongamano hilo ambalo lengo lake kuu ni kujenga utawala bora. Mongela amefungua kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba ambaye pia alikuwa akimwakilisha Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango.

Mongela alisema serikali ya Tanzania imeweka juhudi kubwa katika kuhakikisha ngazi zote zinakuwa na utawala bora unaozingatia uwazi na uwajibikaji kwenye mifumo yote na sekta zote.

Alisema utawala bora, uwazi na uwajibikaji unaanzia kwenye bajeti, usimamizi wa matumizi, mapato ya serikali lakini pia kuwa wawazi ni wadau wote wawe na uwezo wa kupata taarifa bila urasimu.

Alisema kwa dhamira moja watahakikisha rasilimali za taifa ambazo viongozi wamepewa dhamana ya kusimamia kwa niaba ya wananchi, zinasimamiwa vizuri na wananchi wanaona wazi faida ya dhamana hiyo na maendeleo ya nchi kuwagusa moja kwa moja.

Mwananzuoni mbobezi wa masuala ya uchumi Afrika, Profesa Patrice Lumumba, kwa upande wake aliyataka mataifa ya Afrika kuendelea kudumisha ushirikiano kwa vitendo ili kuchochea maendeleo ya nchi hizo kupitia misingi ya uwazi na uwajibikaji.

Akizungumza katika kongamano hilo lililojumisha asasi mbalimbali za kiraia kutoka ndani na nje ya nchi, Profesa Lumumba alisema iko haja kwa viongozi na wananchi wa Afrika kushikamana ili kuwa na matunda ya pamoja.

Prof. Lumumba anashusha nondo nzito kuhusu nchi za Afrika zinavyowategemea waliokuwa wakoloni kupambana na janga la corona kwa kutumia mbinu za wakoloni hao kutatua matatizo ya Afrika.

Kiukweli, Prof. Lumumba anaponda Afrika inavyoamrishwa juu ya nini cha kufanya na Shirika la Afya Duniani (WHO), uamuzi unaotolewa kutoka Geneva, yaliko makao makuu ya taasisi hiyo. Bila kuuma maneno anasema huo ni mwendelezo wa ukoloni mamboleo.

Prof. Lumumba anaunga mkono hatua za aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati John Magufuli za kuacha uoga na kujikataa.

Anasema juhudi za Afrika kupambana na corona hazifanyiki kwa umoja, hivyo kusababisha kutokuwa na kauli moja.

Anapinga suala la Ulaya, mtu akichanjwa nchi moja, unakuwa huru kusafiri nchi zote za Umoja wa UUlaya (EU) lakini Afrika mtu akichanja na kupimwa Kenya, kuingia Tanzania, lazima apimwe tena hata kama ametumia dakika 30 tu kutoka Nairobi mpaka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), Tanzania.

Anatolea mfano wa mti ambaye hakuruhusiwa kuingia, akalazimika kusubiri saa nzima kupimwa tena. Hiyo pia iko kwa mtu kutoka Tanzania kuingia Uganda, Kenya, Rwanda, Burundi na Sudan. Wazungu hawapimi kuingia kila nchi, ukipima nchi moja ya EU, majibu yako yako nchi zote za EU, sasa kwa nini hilo halipo kwa nchi zetu?

Naye Waziri wa Madini, Dotto Biteko anasema Tanzania ni miongoni mwa mataifa yaliyobarikiwa kuwa na rasilimali nyingi muhimu kwa maendeleo ya uchumi yakiwamo madini lakini suala la uwazi na uwajibikaji ni chachu ya kuongeza wawekezaji katika rasilimali hizo.

Biteko anasema mikataba yote ya rasilimali za taifa, iko huru kuonwa na wabunge na hata mwananchi yeyote ila kuna taratibu za kufuatwa.

Kundi la vijana nalo halikuachwa nyuma. Joyce Nkini, Mkuu wa Kitengo cha Masuala ya Uchunguzi na Udhibiti wa Majanga barani Afrika, anaeleza nafasi ya vijana.

Alisema bara la Afrika linatajwa kuwa Miongoni mwa mabara ambayo uchumi wake utakua maradufu endapo ushirikiano wake utadumishwa kwa vitendo na kupunguza utegemezi.

**pascomayalla@gmail.com**
**0754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Hebu tuipe Sayansi nafasi yake jamani



Na Joseph Kulangwa

**Na hata katika mitihani tuliyokuwa tukifanya, iwe ya majaribio ya wiki, mwezi au muhula au mwaka, maswali hayo yakiletwa na kila tulipojibu hivyo, tulikuwa tukipata vema na kuwekewa alama.**

TUKIWA shuleni wadogo tu, wanafunzi wa sekondari, tulifundishwa katika sayansi jinsi mvua inavyopatikana. Tena tukiambiwa kuwa inatokana na maji, yaani mvuke unaochemka ardhini kisha kupanda juu na kutengeneza mawingu na mvua kunyesha.

Tukawa tunaonyeshwa na walimu wetu maabara, tukitumia 'bansen burner' (msioijua hii leo mtakoma). Tukiiwasha kama kibatari hivi na kuchemsha maji kwenye 'test tube' (mtakoma walahi). Humo ndimo tulivyokuwa tunaona mvuke ukipanda baada ya maji kuchemka.

Tulivyokuwa tunafunika kuzuia mvuke ule kutoka nje, vifuniko vilionyesha maji yakidondokea kwenye 'test tube'. Hapo ndipo tulipokuwa tukiambiwa na walimu kuwa mvuke ukishafika angani kwenye baridi kali, basi huganda na kutengeneza wingu ambalo nalo baadaye likiyeyuka husababisha mvua.

Na hata katika mitihani tuliyokuwa tukifanya, iwe ya majaribio ya wiki, mwezi au muhula au mwaka, maswali hayo yakiletwa na kila tulipojibu hivyo, tulikuwa tukipata vema na kuwekewa alama. Tulikuwa tukifaulu masomo hayo kutokana na kujibu vizuri.

Ni matumaini yangu kwamba hata leo mafundisho ni hayo hayo shuleni kuhusu ni namna gani mvua inapatikana. Bado walimu wanasema inatokana na evaporesheni (mnaelewa?). Hiyo ndiyo ilikuwa ikifanyika na ndiyo inayofanyika hadi leo, na mvua kunyesha.

Hivyo maji ya baharini, ya ziwani, ya mtoni, ya mabwawani ya vidimbwini, yakichemshwa sana na miale ya jua, hupanda juu kwa njia ya mvuke, na hiyo ndiyo evaporesheni na kwenda kuunda mawingu yanayozalisha mvua. Hakuna mwujiza mwingine hata akwambie nani.

Pengine mtoto wa chekechea ndiye anaweza kuambiwa kuwa hiyo mvua ni maji yanamwagwa na Mungu hasa baada ya kuaminishwa kuwa Mungu anaishi mbinguni juu. Lakini kwa msomi ataamini katika mchakato wa evaporesheni, hakuna kingine.

Sasa tunapojikuta katika ukame kama huu unaotunyemelea na kushuhudia upungufu wa maji kutokana na mvua kugoma, tukaanza kuhanikiza kufunga kula na kuomba eti mvua inyeshe, tunakuwa tunaitweza Sayansi kabisa, kwamba aliyeibuni alikosea.

Tukae chini tujiulize, kwa nini haya mambo ya ukame yanatokea, kwa nini joto ni kali, kwa nini jua limekasirika? Majibu utaambiwa ni mabadiliko ya tabianchi. Ni Sayansi tu hiyo, hakuna zaidi ya hapo.

Mabadiliko ya tabianchi hayatokani na watu kumchukiza Mungu kama wanaovyotaka kutuaminisha wengine. Hayatokani na Mungu kutaka kuadhibu watu wake. Si kweli, ni Sayansi tu ndiyo inasababisha majanga yote haya, kama tusipoizingatia kila siku tutalia na ukame na ukosefu wa maji na hata umeme.

Watanzania tunaanza polepole kuikataa Sayansi na kuanza kujiingiza katika mambo ya kuamini miujiza. Ona siku hizi kuna manabii na uongo wanajiita maaskofu na walokole, wanaojidai kuponya watu kwa kuwaombea tu madhabahuni.

Wameibuka wanajenga makanisa na masinagogi kwa ajili hiyo, huku zamani wakipanga watu wenye magongo na kupanda majukwaani kuwaombea na kisha kutupa huko magongo na kutembea. Na kutamba wameponesha walemavu wanatembea.

Wakapangwa wengine kufunga macho kwa gundi na kisha kunawishwa na kuona, eti kutokana na askofu fulani kuwaombea! Eti fulani alikuwa kipofu na sasa anaona. Kuaminishwa huku kukatufanya siku moja tukaaminishwa kuwa tunaweza kufunga siku tatu na kuomba kufukuza UVIKO-19.

Watu tukaaminishwa kuwa UVIKO-19 kweli ameondoka kwa maombi. Wacha aanze kutufyeka tena kwa hasira, wenyewe tukarudi kwenye barakoa, maji tiririka na sabuni na kujitenga. Haya ni mambo ya kuaminishana kubeza chanjo na kujiingiza kwenye nyungu, ah jamani!

Leo tunaambiwa tumwombe Mungu alete mvua. Mara nyingine tunaweza kufanya hivyo na kuaminisha watu tuonapo wimbi linajijenga angani, na kuwaambia haya tuombe sasa na kweli wimbi linaachia na mvua inanyesha na hivyo kuamini kuwa Mungu kafanya yake.

Ikiwa hivyo na wanetu wakaamini hivyo, je, kwenye mtihani wa evaporesheni wakiambiwa mvua kisayansi inatengenezwaje wakasema ni kutokana na maombi kwa Mungu, watakuwa wamekosea au wamepatia? Tutafakari jamani.

**Alamsiki!**

SAFU

## KONA YA UKWELI

# Kazi ya siasa si uongo, wanasiasa watambue



Na Thobias Mwanakatwe

**Lakini wanasiasa lazima wafahamu kuwa uongo ni tamko lisilo kweli linalotolewa kwa makusudi. Mtu anayesema uongo anajua au anahisi ya kwamba maneno yake si ya kweli lakini anataka msikilizaji wa maneno yake (au mpokeaji wa ujumbe wake) ayaamini kuwa kweli.**

WIKI hii wajumbe wa Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa wakiongozwa na Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, walianza ziara ya kichama katika mikoa ya Kagera, Geita, Kigoma, Katavi na Tabora.

Kilichonivutia katika ziara hiyo ni kauli iliyotolewa na Chongolo ambayo nadiriki kusema haijawahi kusemwa hadharani na kiongozi yeyote mkubwa kutoka chama kikubwa cha siasa.

Chongolo akiwa katika ya Wilaya ya Muleba Novemba 14, mwaka huu, katika kikao cha shina, alikemea tabia ya baadhi ya viongozi wa kisiasa kuendekeza uongo, fitina, majungu, umbea na kusingiziana. Aliwakumbusha kuwa kazi ya siasa ni kupendana, kushikamana na kuneneana mema.

Katibu Mkuu alilazimika kuyasema hayo baada ya kupokea taarifa ya viongozi mbalimbali wa wilaya hiyo walioanza kusemana vibaya na kujengeana fitina ikiwa ni maandalizi kuelekea uchaguzi mkuu wa ndani ya chama mapema mwakani.

Sasa kauli hii ya Katibu Mkuu wa CCM nadhani itakuwa imefungua ukurasa mpya kwa wanasiasa kwa kuwa siasa si kusema uongo ndipo ufanikiwe. Wapo viongozi wengi ambao wanapenda kusema ukweli na kuwaeleza wananchi ukweli wanapoona jambo fulani haliwezi kufanyika kwasababu moja mbili tatu.

Mfano mzuri ni aliyekuwa Rais wa awamu ya tano, Hayati Dk. John Magufuli. Alikuwa si mtu wa kusema uongo kwa wananchi au wapigakura ili apate mafanikio kisiasa bali alisimama katika ukweli akisena hiki hakiwezekani na anataja sababu.

Aina hii ya viongozi wasiotaka kuwapaka mafuta wananchi hata katika mambo ambayo hayawezekani kufanyika, inapaswa kuigwa na wanasiasa wa sasa hususani vijana kwa kusema ukweli kwa wapigakura wao.

Ninachokiona hii tabia ya baadhi ya wanasiasa kupenda kusema uongo ili kujinufaisha kisiasa itaendelea kukoma taratibu kwa sababu uelewa wa wananchi hivi sasa unazidi kuwa mkubwa kulinganisha na huko tulikotoka.

Baadhi ya wanasiasa wanapenda uwongo kama turufu kwao mara nyingi wamekuwa wakifanya hivyo kipindi cha kuelekea uchaguzi mkuu au uchaguzi ndani ya chama.

Nakupongeza Katibu Mkuu CCM kwa kulitambua hilo mapema ili kama kuna baadhi ya watu walikuwa na mpango wa kupanga uongo ili wachaguliwe, itakuwa imekula kwao.

Pengine wanaoendekeza uongo katika siasa hawafahamu nini maana ya siasa. Siasa ni njia ya kufanya uamuzi katika ngazi mbalimbali za jamii, kama vile mji, taifa au hata dunia nzima.

Katika demokrasia kila mtu ana kiasi fulani cha nguvu, kwa hiyo siasa ya demokrasia ina maana ya watu wote kuchangia uamuzi. Fikria kama wewe kazi yako ni kusema uongo utatoa uamuzi gani?

Lakini wanasiasa lazima wafahamu kuwa uongo ni tamko lisilo kweli linalotolewa kwa makusudi. Mtu anayesema uongo anajua au anahisi ya kwamba maneno yake si ya kweli lakini anataka msikilizaji wa maneno yake (au mpokeaji wa ujumbe wake) ayaamini kuwa kweli.

Mara nyingi uongo hutumiwa kwa kusudi la kuficha kosa, aibu au tendo haramu. Kusudi lingine ni kujipatia faida au kuzuia hasara. Uongo hutazamwa kuwa tofauti na maneno yasiyo kweli lakini msemaji hajui kwamba si kweli au alikosea mwenyewe.

Pia upo uongo usiomuudhi mtu lakini unaokoa uhai wa mtu, uongo usiomuudhi mtu na unaokoa heshima ya mtu na uongo usiomuudhi mtu na kumsaidia mtu.

Uongo alioubaini Chongolo huko Muleba unatoa picha kuwa uko katika maeneo mengi kwa wanasiasa wa ndani ya chama chake na hata katika vyama vingine vya upinzani.

Kwa msingi huo viongozi wote ambao wanapenda kuufanya uongo kama turufu kwao kisiasa, sidhani kama watafaa katika chama kikongwe kama CCM chenye historia kubwa barani Afrika.

Ukisoma katiba ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 1977 ahadi za mwanachama, ya 11 inaeleza kuwa mwanachama wakati wote ni mfano wa tabia nzuri kwa vitendo vyake na kauli yake, kuwa mwaminifu na kutokuwa mlevi au mzururaji.

Sasa kama kiongozi tabia na vitendo vyako ni vya kusema uongo nadhani hapo kama bado upo ndani ya chama tawala huu sasa ni muda wa kujitafakari kama unafiti au la.

Na kwa mwanaCCM yeyote ambaye bado ataendelea kuwa na fikira za kwamba uongo ndio utamfanya aendelee kuchaguliwa katika uchaguzi ujao ndani ya chama, ajue kwamba yuko katika 'danger zone' maana wapigakura sasa watasimamia kauli hii ya Katibu Mkuu.

Isitoshe Katibu Mkuu akiwa wilayani Chato ameshatoa msimamo kwamba uchaguzi wa 2022 ndani ya chama wanataka wagombea wenye sifa. Sasa kama wewe sifa yako ni kusema uongo, nakushauri usiende kuchukua fomu kwa kuwa utaaibika.

Kwa mantiki hiyo, wanasiasa wanaopenda uongo watambue kuwa uchaguzi wa mwaka 2022 wa ndani ya chama na uchaguzi mkuu mwaka 2025 hawatatoboa.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA**

**Kwa maoni na ushauri: Email; mwanakatwe2005@yahoo.com**

## DARASA LA NDOA

# MALEZI YA WATOTO NI JUKUMU LA WANANDOA WOTE



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

**Mtoto mwenye malezi mabaya atakuwa na maisha mabaya hapo mbeleni. Watu wasiowajibika, magaidi, vibaka, walevi, kundi la watoto linalojiita, "watoto wa Ibilisi"kama ilivyoripotiwa na vyombo vya habari hivi karibuni, wahuni wa kila aina tulionao leo ni matunda ya malezi mabaya.**

FAMILIA ni msingi wa maadili mema katika jamii na taifa. Maendeleo yoyote yanahitaji watu waadilifu na uadilifu huo unajengwa kuanzia ngazi ya familia. Tunaishi katika jamii ambayo kuna ombwe kubwa la malezi, hali inayoathiri makuzi ya watoto kwa kuwa tabia na mienendo yetu inajengwa katika familia.

Wanasaikolojia wanasema zaidi ya asilimia 60 ya wewe na mimi tulivyo leo ni matokeo ya makuzi wakati wa utoto. Ni vyema ieleweke wazi kuwa jukumu la kujenga jamii na taifa au kulibomoa, tunalo sisi wazazi, walezi na wanajamii.

Mtoto ni malezi. Malezi bora ni ufunguo na urithi wa maisha kwa mtoto. Kanisa, jamii na taifa bora la kesho, linategemea malezi bora yanayotolewa na taifa bora la leo. Malezi bora ndiyo mwelekeo sahihi wa maisha ya mtoto kwa kuwa kesho bora ya mtoto inajengwa na leo bora ya wazazi bora. Watoto wa leo ni raia na viongozi wa kesho; ndio watakaokuwa sifa au aibu kwa wazazi wao, kwa familia yao, kwa jamaa na taifa lao.

Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo. Wazazi msikwepe wajibu wa kukemea pale inapobidi. Watoto wote wasioadabishwa na wenye tabia mbaya ni udhia, mzigo, karaha, na fedheha kwa wazazi na jamii. Ukimdekeza mwanao iko siku atakuaibisha na kukusababishia maumivu usiyoyatarajia.

Mtoto mwenye malezi mabaya atakuwa na maisha mabaya hapo mbeleni. Watu wasiowajibika, magaidi, vibaka, walevi, kundi la watoto linalojiita, "watoto wa Ibilisi"kama ilivyoripotiwa na vyombo vya habari hivi karibuni, wahuni wa kila aina tulionao leo ni matunda ya malezi mabaya.

Wazazi msiridhike tu na kule kuwapatia watoto wenu mambo ya ulimwengu huu. Watoto wenu wanahitaji uwepo wenu wakionja hisia, mapigo ya mioyo yenu, hali ya kujali na kuthamini maendeleo ya kiroho, kimwili, kiimani, kisaikolojia na kadhalika.

Upendo na muda unaopatikana kwa ajili ya watoto wenu ni zawadi kubwa isiyoweza kuthaminishwa na chochote. Mtoto hahitaji tu baba ila baba mzazi na sio mama tu ila mama mzazi. Baba na mama wasiwe kiwanda cha kuzalisha watoto pasipo kuwajibika katika malezi.

Kuwa baba au mama ni jukumu kubwa. Kwa hiyo, ni muhimu sana wazazi wafahamu majukumu waliyonayo kwa watoto wao ili kujenga familia bora. Maadili ya viongozi yanajengwa kuanzia katika ngazi ya familia. Hivyo, ili tuwe na viongozi bora na waadilifu, lazima mkazo uwekwe katika malezi ngazi ya familia.

Watoto waliozaliwa kama raia wa dunia hii wanapaswa kutambua kuwa uraia wao halisi uko mbinguni. Hivyo lazima waandaliwe kwa ajili ya hatima hiyo pia. Kuwaandaa ni jukumu la wazazi. Ukiwa mzazi au mlezi unaalikwa uwashirikishe imani yako kuhusu Mungu, upendo wako kwa jirani na tumaini la maisha mema ya baadaye.

Tuwape watoto wetu uhuru wa kuamua, kuchagua, kutoa mawazo kuhusu maisha yao, lakini wapewe uhuru wenye mipaka. Uhuru usio na mipaka matokeo yake ni vurugu, fujo na uharibifu. Tuwasaidie watoto na vijana wetu wasiendekeze tamaa starehe na anasa, kiu ya mali na utajiri pasipo uwajibikaji wa kutosha.

Tuwasaidie kufahamu kuwa maisha mazuri yanatengenezwa kwa kuwa na nidhamu binafsi ya maisha, juhudi, subira na uvumilivu na kumtanguliza Mungu katika kila jambo.

Familia iwe ni shule ya Neno la Mungu na sala; ni kitalu cha maadili na maisha mema. Wazazi tuwe mfano mwema wa kauli na matendo mema kwa watoto wetu, kwani watoto hujifunza zaidi kwa kuona. Ikumbukwe kwamba matunda mema hutoka katika mti bora.

Watoto wema hutoka kwa wazazi bora kwa kuwa tunda halianguki mbali na mti wake. Watoto wenye malezi bora; walioelimishwa kumcha Mungu watakuwa na utii, upendo, na msaada mkubwa kwa wazazi wao katika umaskini na uzee wao. Watoto hao watakuwa faraja katika ugonjwa na mateso, furaha ya familia, jamii na taifa.

● Dk. Mlyuka ni mchungaji **wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

# MAISHA

NOVEMBA 21, 2021

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




Ukurasa 14


## Usiwe tipwatipwa, Punguza kula ovyo



Ukurasa 15


## NYUMBA:

Sababu za nyumba kuvuja muda mfupi




## KATUNIKA


Ukurasa 16




# Pambana joto lisiharibu ngozi yako

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | U | H | U | R | U |
| ■ | T | ■ | ■ | A | ■ |
| M | W | A | ■ | S | ■ |
| ■ | A | ■ | D | U | A |
| ■ | N | ■ | ■ | L | ■ |
| B | A | I | N | I | ■ |


## AMSHA AKILI




## TOA TOFAUTI 5



## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
UMA, BAA, KATWA, NYAMA, MWAMBA, NYANYA

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Juma alikwenda sokoni kununua bidhaa akiwa na mama yake, walipofika walianza kununua vitu na kisha walikwenda katika soko la kuuzia samaki. Juma aliwaona samaki wakavu aina ya kambale wakiwa wamekaushwa katika hali ya vipande.

Baada ya kuona hivyo, Juma alimwangalia mama yake na kisha alimuuliza.

Juma: Hawa ni kambale?

Mama: Ndio mwanangu,samaki hawa wazuri wana nyama nyingi

Juma: Lakini mbona hawajakunjwa?

Mama: Wamekatwa vipande hawa

Juma: Kwa hiyo walishindikana kukunjwa wakiwa wabichi, maana mwalimu alisema Kambale mkunje angali bado mbichi.

Mama: Hapana mwanangu huo ni msemo tu, unamaanisha mtu anafunzwa mambo mema akiwa bado mtoto.

**SWALI**

MDUDU kunguni anapatikana sehemu gani ndani ya nyumba?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Migogoro ya Maisha tunaitengeneza sisi wenyewe!

KARIBU tena msomaji wangu. Bado tunaendelea na mada yetu kuhusu vyanzo vya migogoro vinavyotesa maisha yetu ya kila siku. Ipo migogoro binafsi, mingine ikitokana na mazingira tunayoishi. Fuatilia Makala hizo uelimike.

Kuwa na marafiki ni jambo jema. Lakini ni vizuri pia kuangalia watu unaohusiana nao iwe ni marafiki na hata wapenzi. Yamkini unaye mtu umehusiana naye kwa muda mrefu sana. Na ukiangalia na kupima mzani kwa muda ulioishi naye, huwezi kuona faida bali hasara tu. Jiulize, kwa nini upo hapo?

Tatua mgogoro naye, hama. Huwezi kumchukia mtu ambaye mmekuwa na ushirikiano hapo mwanzo. Mshukuru Mungu kwa kuweza kukusaidia kumfahamu. Hauhitaji kutengeneza kisasi wala chuki wala kutengeneza ile hali ya kukufanya wewe ukose amani ya moyo.

Hebu fikiria, hivi ikitokea ukaanza kuishi kwa amani na kufurahia kile ambacho unakifanya, nini kitatokea? Bila shaka ni furaha. Hivyo ni vizuri kama utaanza kujua hivyo leo na kuhakikisha kuwa marafiki unaokuwa nao wana faida kwako.

Mtaalamu mmoja wa saikolojia nikamsikia akizungumza redioni akasema kwamba watu wanahitaji marafiki wa aina tano. Unahitaji marafiki ambao wana taaluma kama yako. Unahitaji marafiki ambao ni wa kiroho kukujenga kiimani. Pia unahitaji marafiki wale uliokutana na hata ukubwani. Si lazima wale mliokuwa nao utotoni.

Lakini pia kuna marafiki wa maisha, yaani uliokuwa nao tokea utotoni. Hawa watakushuhudia wewe, watasema tunamfahamu mtu huyu. Ameishi sehemu fulani na wazazi wake ni akina fulani. Lakini cha ajabu ni kwamba watu wengine wanapopanda viwango kimaisha huwasahau hawa marafiki wa tokea utotoni.

Hawa ni marafiki wa muhimu sana kwa kuwa mwisho wa siku ndio wanaokujua wewe vizuri na ndio watakaokushuhudia wewe vema zaidi. Lakini jambo jingine tunawahitaji marafiki wa kufurahia nao (social friends), kukuchangamsha, wacheshi. Hii ni kwa sababu maisha yamebeba vitu vingi. Raha ya maisha ni kuishi maisha ya furaha ila uwe makini.

Chanzo kingine cha migogoro ni suala zima la mazingira unayoishi. Wapo watu wanapenda sana fedha. Unaweza kumpunja au kumdhulumu au imetokea tu hali fulani inayoashiria mgogoro, inakuwa hapatoshi.

Watu wa aina hii kwao maisha bila fedha hayaendi. Hebu fikiria ukaanza kuishi bila fedha maisha yako yatakuwaje. Kama nilivyoeleza kwenye makala wiki iliyopita sisi ni jumuiya tunahitajiana. Kwa hiyo unahitaji pia watu kuanza kutatua migogoro yako kwanza ili maisha yako yaweze kwenda ipasavyo.

Kwenye mazingira pia kuna eneo fulani upo, yawezekana ni kazini. Umeajiriwa kazini pengine umeletwa na ndugu yako. Sasa kwa sababu umewekwa na haujahangaika mwenyewe unaanza kuwasumbua watu. Unachelewa kufika kazini, unavaa unavyotaka, unakuwa jeuri. Yaani wewe unaharibu- haribu tu mambo.

Kwa nini utengeneze migogoro ya watu wengine. Mwisho wa siku watu wanaanza kukuchukia na pengine wanaanza kukutengenezea mipaka wakiona wewe ni tatizo. Sasa wewe si tatizo bali ni faida. Kwa hiyo ni vizuri ukahakikisha mazingira uliyopo sasa yanakuwa ni baraka kwa watu wengine.

Hakikisha unatatua migogoro ya mazingira yako uliyopo. Hakikisha unapunguza ile hamasa uliyo nayo ya kupenda vitu fulani vinavyosumbua watu wengine. Kila mtu ana haiba yake. Wapo watu ambao ni wapole na wengine ni wacheshi sana.

Inapotokea wewe ni mpole sana, lazima uweze kufahamu utofauti wako. Fahamu madhaifu yako na fahamu pia changamoto zako. Wapo watu hawafahamu wao wana udhaifu gani.

Kama udhaifu wako ukivua viatu miguu inanuka, elewa hivyo. Kwamba sitaki kuwa wengine shida, hivyo usivivue! Ni kujielewa na kufahamu udhaifu pamoja na uwezo wako. Kama unajielewa mimi naweza kufanya kitu fulani, wewe fanya ili mwisho wa siku watu wengine waweze kufaidika kutoka kwako.

Upo muda pia unapaswa kuvielewa vitu vidogo vidogo kwa sababu hiyo ndio hekima yenyewe. Ndio maana mtu mwenye hekima anaweza kujifunza jambo jema kupitia jibu la mtu ambaye hana hekima. Hata wewe msomaji wangu naamini kipo kitu unajifunza leo.

**Niishie hapa, wiki ijayo tutaona usaliti kama aina nyingine ya mgogoro. Je, una maoni, kisa cha kimaisha? Tuma ujumbe kwenye 0715268581.**

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Mabadiliko ya tabia nchi yatufundishe kuheshimu sheria

KILIO cha mgawo wa maji kimetawala kila mahali kwa sasa na mamlaka za maji zimewataka wateja kuwa waangalifu kwa kuwa kiwango cha maji kimepungua.

Dar es Salaam, mgawo ulianza wiki iliyopita, huku Morogoro wakitahadharisha kuwa iwapo mvua hazitanyesha ndani ya siku 21, basi makali ya mgawo wa maji yataongezeka.

Pia Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), limetoa taarifa ya kupungua kwa maji kulikoathiri vyanzo vya maji vya Kihansi, Kidatu na Pangani, kulikopunguza uzalishaji kwa megawati 345 sawa na asilimia 21.

Aidha, wamesema jitihada zinafanyika ili kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kutumia gesi ambazo ni megawati 358 zitakazokidhi mahitaji, huku likiwaomba radhi wateja kwa usumbufu utakaojitokeza na kwamba taarifa zitatolewa kwa baadhi ya mikoa ili wapange kazi zao.

Kila mamlaka inasema sababu kubwa ni mabadiliko ya hali ya hewa yaliyopunguza maji kwenye vyanzo mbalimbali ikiwamo mito.

Tayari Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imeeleza nchi inakabiliwa na jua la utosi mikoa ya Kilimanjaro, Ruvuma na Dar es Salaam ikiongoza kwa joto kali.

Pia Rais Samia Suluhu Hassan ameagiza kukamatwa kwa wanaochepusha maji kwa ajili ya kilimo na mifugo na kusababisha watumiaji wengine kukosa kukamatwa na kuchukuliwa hatua kali.

Haya yote yanapaswa kutukumbusha sheria ya mazingira ambayo inazuia shughuli zozote za kibinadamu kwenye chanzo cha maji kwa umbali wa mita 60.

Leo hii hali ikoje kwenye vyanzo vya maji? Watu wanafanya shughuli za kilimo hadi kwenye vyanzo na hata pale ambako ndiko chemchem ya maji kumeharibiwa na watumiaji hasa mifuko na shughuli za kilimo.

Kwa sasa ni kawaida kukuta watu wanachepusha chanzo cha maji ili kuweka makazi au kufungua mashamba, hali hii inasababisha madhara makubwa ambayo huumiza wengi zaidi.

Ni lazima kama nchi kuwa na utaratibu wa kulinda vyanzo vya maji pasipokuangaliana usoni na kuoneana aibu kwa kuwa yakija madhara kama tunayoyaona sasa ndiyo shida ya maji kwa ajili ya matumizi ya kawaida na watumiaji wengine kama wakulima na wanyama inazidi, huku kwenye kuzalisha umeme yakipungua zaidi.

Madhara ni makubwa na ya muda mrefu lakini uharibifu huanza taratibu na wakati hayo yakiendelea mamlaka za kusimamia sheria zipo na zinaona, lakini wakati mwingine inakuwa nje ya uwezo wao kwa kuwa wanasiasa hujitokeza kwa nguvu kulinda wanaowaita ni wapiga kura wao.

Mathalani, ukitembelea kando ya Mto Ruvu, utaona shughuli za kilimo zilivyoshika kasi ambazo haziishii kuathiri upatikanaji wa maji pekee bali hata ubora wa maji.

Kilimo kinachofanyika ni cha mbolea na dawa mbalimbali ambazo husafirishwa kwa maji kwenda kwenye mto na hayo watu wote huyatumia kwa matumizi mbalimbali ikiwamo kunywa.

Kama kuna madhara ya kiafya wanayayapata watu wote waliosababisha uharibifu na wasiohusika kabisa, lakini lawama kubwa inaelekezwa kwa wenye mamlaka ambao walipaswa kusimamia vyema sheria zilizopo.

Ni muhimu sana wananchi wakaelimishwa na sheria kuchukua mkondo wake katika kukabili wanaofanya shughuli za kilimo ndani ya mita 60, kuendelea kuwaacha hakuishii kupunguza maji pekee bali madhara ya kiafya kutokana na kemikali zilizotumika.

Ni muhimu pia mamlaka husika zikaangalia kwa umakini suala la uchafuzi wa maji kwa kuwa ni maumivu kwa wengi hasa kwa maradhi ya saratani na mengine ambayo hayana tiba.

Bila kuwa na mipango endelevu ya kulinda vyanzo vya maji ukame utaendelea kuitesha nchi, licha ya kwamba ni janga la dunia, lakini kukiwa na mikakati bado wananchi hawataumia kwa kukosa umeme na maji safi na salama.

Muhimu zaidi ni wananchi kufundishwa kuwa na akiba ya maji kwa kuvuna maji ya mvua ambayo huachwa kuingia ardhini tu.

Kuna taasisi mbalimbali kama shule, huduma za afya, magereza na ofisi za umma zenye majengo makubwa ambazo zinaweza kuvuna maji na kuyatengeneza kwa ajili ya matumizi ya muda mrefu hasa wakati wa ukame kama sasa.

Mwaka jana nyakati kama hizi ilikuwa ni wakati wa mvua lakini kwa mwaka huu ni wakati wa jua kali kama la mwezi wa tisa, hii ni ishara kuwa mambo hayako vizuri na tunawajibu wa kutunza mazingira kwa faida yetu na vizazi vijavyo.

**Mungu ibariki Tanzania**











Oktoba 30, mwaka huu, ilikuwa siku ya furaha kwa familia ya John Thobisa Mlay baada ya kufunga ndoa na Luindeni Frank Kisanga katika kanisa la Katoliki la Mwenyeheri Anuante , Parokia ya Makuburi jijini Dar es Salaam. Sherehe ya kuwapongeza maharusi ilifanyika katika ukumbi wa Mwika.

MITINDO



Na Moshi Lusonzo

# TUPIA HIVI
## Kipindi hiki cha joto

TANZANIA ni miongoni mwa nchi zinazopata athari za moja kwa moja za mabadiliko ya tabia nchi kwa kuwa na kiwango cha juu cha hali ya joto.

Kuongezeka kwa joto hata mwenendo wa maisha ya watu hubadilika, na moja ya vitu vinavyoonekana kubadili mwenendo ni suala zima la mavazi.

Katika kipindi hiki cha joto, baadhi ya mavazi ni vigumu kutumia kutokana na mwili kushindwa kuhimili na ndio maana watu wanatakiwa kuwa makini na kuchagua aina sahihi ya nguo.

Kulingana na ushauri wa wataalamu wa mavazi, nguo sahihi zinazotakiwa kuvaliwa katika kipindi cha joto ni zile zenye uwezo wa kupitisha hewa vizuri na zenye rangi zinazoakisi mwanga.

NGUO GANI UVAE KIPINDI CHA JOTO?

Aina ya mavazi yanayopendekezwa kuvaliwa kipindi cha joto kali ni zile za pamba, Hariri na mchanganyiko wa sufi nyepesi.

Kama mpenzi wa magauni marefu, unatakiwa kuvaa lenye kitambaa chepesi na halina mikono mirefu, ili kuufanya mwili uweze kupumua vizuri.

Wanaopenda magauni mafupi, wanatakiwa kuzingatia kuishia katika magoti na juu lisiwe na mapambo mengi ya ziada, badala yake mikanda membamba mabegani.

Miguuni usiwe na mbwembwe nyingi ya kuvaa viatu vinavyoziba eneo kubwa la miguu, badala yake kuwa na viatu vya kawaida vinavyoacha nafasi kubwa ya miguu kuwa wazi.



UREMBO

Na Mary Geofrey



# Pambana joto lisiharibu ngozi yako

NGOZI ya mwanadamu inahitaji matunzo ili iweze kuwa na afya na mvuto wake wa asili.

Kama ngozi isipotunzwa vizuri huweza kupata magonjwa kama upele na ukurutu na kupunguza mvuto wa mwonekano.

Hata hivyo, ngozi za watu hutofautiana kutokana na maumbile ya mtu husika, kuna ambao ngozi zao zina mafuta na wengine kavu.

Uzuri wa ngozi sio rangi tu bali ni mwonekano wake kuwa na afya na mng'ao unaoashiria uhai.

Wakati huu wa joto na jua kali, unapaswa kuhakikisha unakunywa maji ya kutosha, kutumia kofia ya kujikinga na kupata muda wa kupumzika.

Pia unatakiwa kutumia njia za asili kwa ajili ya kuitunza ngozi yako na kuifanya kuendea kuonekana maridadi.

Baadhi ya njia za asili ni kuosha uso kwa maji yenye joto la kadri(uvuguvugu) ili kunafungua matundu ya ngozi.

Tumia tango au limao kama kusafisha, kisha tumia taulo safi kujifuta taratibu ili kuondoa uchafu katika ngozi yako.

Kadhalika unaweza kutumia machicha ya nazi kama scrub, ya kuondoa seli zilizokufa na kuifanya ngozi kuwa laini na kuipa mng'ao.

Tumia pia kiini cha yai kama maski, matundu ya ngozi yanajifunga vizuri na kinaipa ngozi yako lishe kutokana na vitamini zilizomo kwenye kiini cha yai kama vitamin E.

Mwishoni nawa na maji baridi ili kuruhusu matundu ya ngozi kujifungua na kuifanya ngozi ijiweke sawasawa.

Faida ya njia hii ya asili ni kutibu na kuikinga ngozi dhidi ya joto.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Usiwe tipwatipwa, punguza kula ovyo

WOTE tunafahamu mpangilio wa vyakula usiofaa husababisha kupata viriba tumbo na magonjwa yasiyoambukiza.

Kwa wale wenye vitambi na miili mikubwa ambayo imekuwa ikiwatesa, wanashauriwa kubadili mfumo wa vyakula ili kurudi katika mwili wa kawaida.

Wanaotaka kupungua siyo vizuri kushinda na njaa, unaweza kutumia aina ya vyakula hivi kupunguza kasi ya kuongezeka mwili.

### Saladi ya Parachichi

Parachichi ni tunda muhimu sana kama unajaribu kupunguza uzito.

Lina virutubisho vinavyopelekea kuchomwa mafuta mwilini zaidi.

Pia unaweza kutumia fursa hii kuongeza mbogamboga na matunda mengine yanayosaidia katika kupunguza uzito. Unaweza kutumia parachichi wakati wowote.

### Namna ya kuandaa

Vipande 4 vya vitunguu vilivyokatwa kwa mviringo, machungwa 2, maparachichi 2, vijiko 3 vya chai vya mafuta ya zeituni (olive oil), vijiko 2 vya chai vya majani ya mint -kijiko 1 cha chai cha maji fresh ya ndimu na kijiko robo cha chai cha chumvi.

Menya machungwa na ondoa kabisa ule weupe ibaki nyama tu. Katakata vipande vya mviringo.

Menya na katakata maparachichi upendavyo, ongeza majani ya mint. Ongeza mafuta ya olive ukipenda kwa ajili ya kuongeza ladha na umwagie maji ya ndimu na tayari kwa kuliwa.

### Juisi ya ndimu na Tikitimaji

Ndimu na tikitimaji vyote ni aina ya vyakula ambavyo vimekubalika kusaidia kupunguza uzito.

Ndimu inatumika katika detox na pia inasaidia kuchoma mafuta zaidi.

Tikitimaji lina maji mengi, mafuta sifuri na nyuzinyuzi sana hivyo lina uwezo wa kushibisha kwa muda mrefu na hivyo kumuepusha mtu kula vyakula vibaya.

Pia nyuzinyuzi zinatumia nishati nyingi wakati wa umeng'enywaji na hivyo huchoma mafuta mengi mwilini na unaweza kutumia wakati wowote.

### Namna ya kuandaa

Ndimu 1 (ikamuliwe), tikiti kipande 1 saizi ya kati (lililomenywa), majani ya mint kiasi (ukipenda) na changanya vyote kwenye blenda na saga mpaka upate kinywaji chenye rangi nyekundu.

Hapo unaweza kunywa moja kwa moja na usichanganye na maji wala usiongeze sukari.



Na Elizabeth Zaya



# Sababu za nyumba kuvuja muda mfupi

## Tumia sehemu ya chini ya ngazi kubuni vitu mbalimbali



KATIKA nyumba nyingi sehemu inapowekwa ngazi inakuwa na nafasi kubwa ambayo haitumiki. Lakini wapo wanaotumia nafasi hiyo kwa kubuni vitu mbalimbali ambavyo vitatumika ndani ya nyumba. Hizi ni baadhi ya dondoo ambazo unaweza kutumia nafasi za wazi katika ngazi.

1: Kitanda cha kupumzikia ni ubunifu mzuri ambao unaweza kuweka sehemu ya chini ya ngazi na kufanya nyumba yako kuwa na mwonekano wa kuvutia.

2: Unaweza kugeuza sehemu hiyo kwa kutengeneza kabati maalum kwa ajili ya kuhifadhia vitu mbalimbali. Hakikisha madroo yake yanaweza kuwa ya wazi au yenye milango ya nakshi.

3: Pia unaweza kubuni kuwa sehemu ya kuhifadhia vitabu na majarida muhimu, sehemu hii inaweza kuwa maktaba yako ya ndani ya nyumba na kuwafanya wanafamilia na wageni kujisomea.

4: Kama wewe mpenzi wa wanyama, sehemu hiyo ya wazi unaweza kujenga chumba cha kulala wanyama kama paka na mbwa. Hakikisha unakipamba vizuri na kuweka kitanda cha wanyama kinachovutia.

KUWA na nyumba bora na imara ni ndoto na furaha ya kila mtu anayemiliki au anayetarajia kumiliki nyumba hiyo.

Lakini inapokuwa kinyume cha matarajio ya kumiliki nyumba ya vigezo hivyo, moyo huinama japokuwa wakati mwingine hali hiyo inasababishwa na kukosea uchaguzi wa wataalamu wa ujenzi wa nyumba husika ambao hujenga chini ya kiwango.

Mtaalam wa masuala ya ujenzi, Abeid Ng`anzi, anazungumzia sababu mbalimbali zinazochangia baadhi ya nyumba kuvuja muda mfupi baada ya ujenzi wake.

Anasema miongoni mwa sababu ni matumizi ya vifaa vya ujenzi vya hali ya chini ambavyo baadhi ya watu hufanya hivyo kwa kudhani kuwa wanaokoa pesa.

Sababu nyingine, anasema baadhi ya vifaa vinavyovaliwa na mafundi wakati wa kuezeka huwa si rafiki kwa paa, hivyo kudhoofisha kifuniko cha paa ambacho baadae hutengeneza ufa na kupitisha maji.

Mbali na sababu hizo, pia anasema paa la nyumba linaweza kuharibiwa na upepo hasa kama halikuezekwa kwa utaalam mzuri, hivyo kuvuja.

Anasema muundo wa paa lenyewe pamoja na makosa yaliyofanywa wakati wa kuezeka na kwamba kwa makosa hayo ya kuvuja kunaweza kutokea hata ndani ya mwaka mmoja baada ya ujenzi wa nyumba husika.


Nyingine anasema ni ufungaji mbaya wa paa wakati wa kuezeka na kwamba kasoro kama hiyo huonekana haraka ndani ya wiki chache baada ya nyumba kuanza kutumika.

"Paa linaweza kuvuja kwa sababu ya ukiukaji wa matumizi ya teknolojia ya ujenzi. Kwa mfano, kitaalam unatakiwa kuweka nyenzo za kuezekea katika tabaka tatu, wewe unaweka tofauti na hapo na makosa mengine madogo yanayofanana na hayo yanayofanywa wakati wa kuezeka," anasema.

Anashauri kwamba njia nyingine ya kuepuka paa lako lisivuje ni kuwa makini kuchagua wataalam wa kukuezekea, kutumia vifaa bora bila kujali gharama, kufuata kanuni zote za uezekaji na kukagua paa la nyumba yako mara kwa mara angalau mara mbili kwa mwaka na kuondoa vitu vyote ambavyo hutuama juu yake ambavyo kwa namna moja ama nyingine hutengeneza nyufa hususani vyuma na vitu vizito.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
JOTO BABUWEE KULALA KUACHIANA NAFASI
KIPELE KIMEMPATA MKUNAJI!
MMEONA SASA!!! SERA ZENU NA SIASA ZENU ZIMESABABISHA KUWEPO KWA UKAME JOTO KALI, MGAO LAKINI TUNGEKUWA SISI YASINGETOKEA HAYA!
UMEFIWA VIPI NA MKE WAKATI UMEANDIKISHA WE' BACHELA?
NAKUMBUKA SIKU NAJAZA FOMU YA AJIRA NILIPITIA BAR KUPIGA VITU! TENA SIKOSEI PIA NILI-JAZA MIE MJANE!
MENEJA MUAJIRI WATU
KAMA HUNA MOYO WA SUBIRA UNAWEZA KUMSUKUMIA MAKONDE!
HA HA HA HAAAAA WAZIMU SIO MPAKA UANZE KUWEHUKA NGUO MKONONI
VITU UNAVYO-NIFANYIA NI UCHURO NIMEJUA LAZIMA KUNA JANGA LITATOKEA TU! TENA KUBWAAA...
UNATAKA KUSEMA HILI 'JOTO KALI' LIMETOKANA NA KUKUTOA AUTI NA KUKUNUNULIA VIJORA KILA WIKI?
BABA VANNILA LEO TUSHINDE TUONGEE MUME WANGU USINIFANYIE HIVYO MWENZAKO! TUKIONESHA UPENDO HATA JOTO HATUTALIONA!
KODI INAPANDA RASMI KUANZIA MWEZI UJAO MSIJE MKASEMA NIMEWASTUKIZA "NDO NSHASEMA IVO!"
LIMEPANDA JOTO NA HATUJASTUKA! ITAKUWA KODI?
HAYO NILIYAJUA! MMEAMKA NA MKEO MMENUNIANA NIKAJUA HASIRA ZAKO LAZIMA ZIJE KWETU! CHEZEA JOTO WEWE!!!
WEWE! WE! WEWE! USTAKE KUNTAFUTA UNDANI! UNANICHEFUA MAMA NANIHIII... OHOOOOO!!!
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...MAJI YA MOTO ASILI YAKE BARIDI...

HABARI KIMATAIFA

## Jeshi Sudan laua watu 40

**KHARTOOM,** SUDAN

IDADI ya watu waliouawa nchini Sudan kutokana na maandamano ya kupinga mapinduzi mwezi uliopita imepanda na kufikia 40.

Taarifa hiyo ni kwa mujibu wa maofisa wa afya baada ya kijana mmoja aliyepigwa risasi kichwani siku chache zilizopita kufariki.

Maandamano hayo yaliyofanyika Jumatano, yaligeuka kuwa ya vurugu na kusababisha watu 16 kupoteza maisha.

Hata hivyo, Polisi wanakana kutumia risasi za moto na kusisitiza kwamba wamekuwa wakitumia nguvu za kawaida kutawanya maandamano.

Juzi, makundi madogo ya waandamanaji yalikusanyika katika vitongoji kadhaa vya Kaskazini mwa Khartoum na kuweka vizuizi barabarani.

Chama cha wanataaluma wa Sudan (SPA), kimewasihi raia kuendeleza kampeni ya kupinga mapinduzi.

Kiongozi wa juu wa kijeshi Abdel Fattah al Burhan, mnamo Oktoba 25, alitangaza kuvunja serikali ya kiraia na kuwakamata viongozi wake.

# Kamala Harris aiongoza Marekani dk 85 wakati Rais Biden akiwekwa nusukaputi

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAKAMU Rais wa Marekani Kamala Harris, ameweka rekodi kwa kuwa mwanamke wa kwanza kupewa mamlaka ya muda mfupi ya kuongoza taifa hilo kubwa kiuchumi na kijeshi, wakati Rais Joe Biden, alipokuwa akifanyiwa uchunguzi wa kiafya.

Harris, mwenye umri wa miaka 57, alikuwa na mamlaka ya uongozi wa nchi kwa kipindi cha dakika 85 wakati Biden alipopewa dawa ya usingizi (nusu kaputi) kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi wa utumbo Ijumaa.

Daktari wa Rais Biden alitoa taarifa baada ya uchunguzi huo, akisema kuwa kiongozi huyo ameamka akiwa mwenye afya na anaweza kutekeleza majukumu yake ya kikazi.

Uchunguzi huo wa kimatibabu ulifanyika siku moja kabla ya Rais Biden kuadhimisha miaka 79 ya kuzaliwa kwake.

Bila kipingamizi makamu huyo wa rais, alitekeleza majukumu hayo katika ofisi yake ya kawaida iliyopo katika jengo la West Wing la Ikulu ya White House, maofisa walisema.

Rekodi nyingine aliyeivunja ni kuwa mwanamke wa kwanza Mmarekani mwenye asili ya rangi nyeusi na Kusini mwa Asia kuchaguliwa kama Makamu rais wa Marekani.

Ofisa wa habari wa White House, Jen Psaki, alisema kuwa kuhamishwa kwa muda wa mamlaka katika hali kama hiyo ni jambo ambalo halikuwa la ajabu, na kwamba ni sehemu ya mchakato uliopangwa na katiba ya Marekani.

"Kama ilivyokuwa wakati Rais George W Bush alipofanyiwa uchunguzi sawa na huu katika miaka ya 2002 na 2007," alisema katika taarifa.

Rais Biden alionekana akitabasamu alipokuwa akirejea Ikulu na alisikika akisema"Nahisi vizuri,"

"Rais Biden ameendelea kuwa mwenye afya, mkamavu, mwanamume mwenye miaka 78, ambaye ana uwezo wa kufanikiwa kutekeleza majukumu yake ya urais ," aliongeza Kevin O'Connor, daktari wa rais huyo.

O'Connor, ambaye ni daktari binafsi wa rais, alisema utumbo wa rais ulionekana umeanza kuwa na uvimbe mdogo ambao ulikuwa rahisi kuuondoa.

Aliongeza kwamba mwendo wa rais ulionekana wa kukakamaa na wa mtu asiye na maji maji ya mwili kuliko siku zilizopita. Hii ilitokana na kuharibika na kupasuka kwa mgono.

Biden, ambaye ni rais mwenye umri mkubwa zaidi kuwahi kuiongoza Marekani, alikuwa amefanyiwa uchunguzi wa mwisho wa kimatibabu mwezi Disemba 2019.

**BBC**



Rais wa Marekani, Joe Biden na makamu wake Kamala Harris.

# Corona yazidi kuitesa Ujerumani, Serikali yatangaza hali ya dharula

**BERLIN,** UJERUMANI

WAZIRI wa Afya wa Ujerumani, Jens Spahn, amesema hali nchini mwake imezidi kuwa mbaya kuliko wiki iliyopita na kuongeza taifa hilo linakumbwa na hali ya dharura ya kitaifa baada ya kuelemewa na maambukizi mapya ya ugonjwa wa Covid-19.

Kauli yake imekuja wakati baraza kuu la bunge la Ujerumani kuidhinisha HYPERLINK "https://www.dw.com/sw/ujerumani-yawekamasharti-mapya-kudhibiti-covid-19/a-59871558" masharti mapya kudhibiti COVID, siku moja tu baada ya bunge kupitisha masharti hayo.

Spahn alikuwa akizungumza na waandishi wa habari akiwa pamoja na Lothar Wieler, Mkuu wa Taasisi ya Kupambana na Maradhi ya Kuambukiza nchini Ujerumani, Robert Koch (RKI).

Akizungumzia kazi ya kuenea kwa ugonjwa huo, Wieler alielezea kuhusu taswira ya kutatanisha ya hali ya maambukizi ya virusi vya corona, na kusema umesambaa katika robo ya wilaya zote nchini humo.

Alisema maambukizi mapya yanaweza kuwafikia watu 500 katika jumla ya 100,000 na kwamba hospitali zinatishiwa kulemewa, hivyo ipo haja kubadilisha hali hiyo.

Wieler alisisitiza umuhimu wa watu kupata chanjo, akieleza zinafanya kazi vizuri zaidi, kuna umuhimu wa kujaza pengo ambalo limeachwa na wale ambao hawajachanjwa.

Katika wiki mbili zilizopita, idadi ya maambukizi mapya imeongezeka kwa zaidi ya asilimia 60.

Juzi pekee, Ujerumani ilirekodi maambukizi mapya 52,970, siku moja tu baada ya kurekodi maambukizi mapya ya watu 65,000, hiyo ikiwa idadi ya juu zaidi kuwahi kurekodiwa nchini humo janga lianze.

Maofisa wa afya wametahadharisha kwamba huenda takwimu hizo zikaongezeka maradufu katika siku chache zijazo.

Uwe Janssens, katibu mkuu wa chama cha wanaowahudumia wagonjwa mahututi alisema idadi ya maambukizi inatia wasiwasi.

Kulingana na mpango mpya, ikiwa zaidi ya watu watatu miongoni mwa wakazi 100,000 wa eneo moja wataambukizwa COVID-19 na kulazwa hospitalini, basi masharti ya "2G" yatazingatiwa katika kumbi zote za starehe na burudani. Na kwamba wale ambao wamechanjwa au wamepona baada ya kuugua ndio wataruhusiwa katika sehemu hizo ikiwamo migahawa na mahoteli.

Ikifikia kiwango cha "2G+" ikiwa idadi ya wagonjwa wanaolazwa hospitalini itafikia 6 kati ya kila watu 100,000 katika eneo moja. Hiyo itamaanisha hata wale ambao wamechanjwa au walioopona baada ya kuugua, watalazimika kupima tena na kuthibitisha kuwa hawana virusi hivyo. Takwimu hiyo ikiongezeka na kufikia watu tisa basi viwango vya juu vya masharti vitatekelezwa.

Kuna hofu huenda hospitali zitalemewa ikiwa idadi ya maambukizi itaendelea kupanda.

Sharti lingine linalochukuliwa ni kupimwa wageni na wafanyakazi wote wanaofanya kazi katika vituo vya kuwahudumia wazee.

MAKALA

# HUDUMA KWA MTEJA



Na Magabilo Masambu

HUDUMA kwa mteja ni dhana ambayo watu wengi huichukulia poa pale wanapohitajika kuitoa kwa yule anayestahili kupata mahala fulani. Watu wengi hudhani kwamba dhana hiyo hustahili tu kutolewa kwa mtu anayefanya biashara na kwamba kama hakuna biashara inafanyika, basi hakuna umuhimu wowote.

Kule kijijini kwetu kwa maana ya nyumbani, kuna kautaratibu ka kumkirimu mgeni anapofika nyumbani. Wakati nikiwa mtoto mdogo, sikuelewa kwa nini nyumba nyingi zikijengwa lazima iwekwe milango miwili, yaani nyuma na mbele. Nikaja kugundua kuwa kumbe mgeni anapofika nyumbani huwekwa upande mmoja wa mlango, hasa nyuma ili kule mbele shughuli za kumwandalia chakula wakati zikiendelea yeye hatakiwi kujua.

Baada ya chakula kukamilika, huku mazungumzo yakiendelea mlango wa nyuma sasa ulitumiwa kuingia ndani, ili kupata chakula alichoandaliwa. Kwa utamaduni wetu, huwa si jambo jema kumuuliza kama ana njaa ama la au kuandaliwa chakula huku akiona ni marufuku kwa sababu kumuuliza au kuandaa wakati anaona anaweza kusema ameshakula, wakati hajala ndiyo maana huwa anaandaliwa chakula bila taarifa. Jambo hili ndilo huitwa ukarimu kwa mgeni.

Huduma kwa mteja pia ni ukarimu maana yake kama mtu hana hulka ya ukarimu kwa vyovyote vile hawezi kutoa huduma nzuri kwa mteja. Wako watu wanaanzisha biashara lakini hazichukui muda zinakufa. Walio wengi wamekuwa wakidhani kwamba wanalogewa biashara zao lakini ukweli ni kwamba wanajiloga wenyewe katika huduma mbovu wanazozitoa kuanzia kumkirimu mteja.

Unaweza kuingia katika mgahawa kwa ajili ya kupata chochote. Unafika unakaa zaidi ya dakika 10 hakuna mhudumu yeyote atakayekuja kukusikiliza. Baada ya muda anakuja tena kwa maringo, unaagiza kinywaji au chakula unakaa zaidi ya nusu saa ulichoagiza hakijaja. Kikifika kitizama hakifanani na bei ulioambiwa unaamua kula na baada ya kula unaagiza bili ya chakula uletewe. Nayo unasubiri kwa muda mrefu wakati mwingine inakulazimu unyanyuke ukamtafute aliyekuhudumia ili umpatie fedha. Unampatia pesa unangoja tena baada ya muda mrefu ndiyo chenji inarudishwa, unadhani huyo mtu atakuja tena kula chakula hapo?

Kuna wakati unakwenda dukani unaulizia bidhaa fulani unaambiwa ipo, unaomba upewe na unapolipa pesa unaambiwa hatuna cheji! Yaani mtu anashindwa kuuza bidhaa kwa sababu hana chenji na anaona kwenda kutafuta ni usumbufu. Ukiondoka anajifariji kwamba huyu mmoja tu hawezi kuleta hasara ngoja aende. Hujui kwamba huyo ndiye balozi wako atawaambia na wengine kuhusu biashara zako.

Eneo lingine ni huduma kwa wateja ofisini. Huku nako hali ni mbaya sana hasa baadhi ya ofisi za umma. Huku kuna kudharauliana. Kabla mtu hajakupokea, anakutazama kuanzia kidole cha mguu mpaka kichwani. Kwa hiyo anakupokea kutokana na unavyoonekana.

Hatari waliyo nayo ni kwamba hujui unampokea nani. Inawezekana kabisa ukampokea mtu vibaya kesho akawa bosi wako au akawa hana nafasi yoyote lakini anafahamiana na mtu ambaye ana mamlaka juu yako.

Kuna baadhi ya ofisi unapokewa kiasi cha kujihisi wewe ndiye mkosaji. Unajiuliza nimekosea nini? Unapokewa kwa kauli ngumu kana kwamba umekwenda kugombana nao. Inagharimu nini kumsikiliza mtu vizuri kama jambo huhusiki nalo unamjibu tu vizuri kwamba, hili si letu au muone yule kwa lugha nzuri ambayo itamfanya awe na amani na kuondoa shaka kwamba inawezekana kuna ajenda nyuma ya pazia ndiyo maana anakaripiwa.

Unaweza kujiona leo unayo nafasi kubwa ya kumjibu yeyote unavyotaka lakini maisha yanabadilika. Uliyemjibu vibaya kuna siku atakuwa bosi wako, halafu ndiyo utajua kwa nini pimbi alikosa mkia wakati mjomba yake ndiye aliyekuwa anagawa mikia. Rais mstaafu Jakaya Kikwete amewahi kusema amewahi kuwa katibu wa Mzee Pius Msekwa akawa anaripoti kwake lakini baadaye Kikwete akawa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hiyo Mzee Msekwa akawa anaripoti kwake.

Ni muhimu sana wakati wa kutoa huduma kumheshimu kila mtu na hasa usiyemjua kuliko unayemjua. Inawezekana kupanda kwako cheo kungetokana na jinsi unavyowapokea watu na kuwahudumia au wengine wamekuletea habari njema unawapokea vibaya wanaamua kutokupatia habari njema hiyo.

Maandiko yanasema Mwenyezi Mungu alipotaka kuiangamiza Sodoma na Gomora aliwatuma malaika kwenda kumpasha habari Lutu kuondoka katika mji ule. Walikuja katika mfano wa binadamu akawakarimu akawapatia chakula na ndipo baadaye wakampasha habari ya kuondoka pale.

Je, ingekuwaje kama angeliwapokea vibaya? Inawezekana wangeliahirisha mpango wao wa kumweleza aondoke. Ndivyo ilivyo hata katika huduma za ofisi na mahali pengine tunaweza kuwafukuza malaika wenye habari njema kwetu kwa sababu ya ujinga au kiburi cha madaraka.

Nafahamu kwamba hulka ya ukarimu si kila mtu anayo lakini tunachotakiwa kufahamu ni kwamba huduma nzuri kwa mteja ni tiba nzuri kabla ya tiba yenyewe.

Ukiwa na tabia ya kukarimu watu vizuri, utafahamu na usiyostahili kuyafahamu yaani unampa mtu nafasi ya kukwambia na mambo mengine ya nyongeza.

Vijana wanasema mtu atafunguka! Ni muhimu watu kufundishwa namna ya kutoa huduma kwa mteja, ili kujenga biashara imara au mahusiano imara kazini au ofisini.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Vituko vya Dk. Remmy na gari yake mitaani



Na Adam Fungamwango

KWENYE safu hii tumeshawahi kumzungumzia mwanamuziki maarufu nchini Tanzania hadi leo, Dk. Remmy Ongalla, alivyokata rufani baada ya kupigwa mweleka kwenye mashindano ya mtu mwenye sura mbaya yaliyofanyika katikati ya miaka ya 1990.

Remmy, ambaye jina lake halisi ni Ramadhani Mtoro Ongalla, aliyezaliwa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, wakati huo ikiitwa Zaire, licha ya kwamba alikuwa mwanamuziki mkubwa na maarufu akiimba nyimbo mbalimbali zilizopendwa na kuchukua tuzo, pia alikuwa ndiye mwanamuziki mwenye vituko zaidi nchini Tanzania kwa wakati huo.

Akishirikiana na wenzake, walianzisha mashindano ya mtu mwenye sura mbaya yaliyofanyika kwenye ukumbi wa Kinondoni Social Hall na kugaragazwa vibaya na kijana mmoja aitwaye Masudi, ambaye baadaye alitambulika zaidi kwa jina la Masudi Surambaya.

Remmy alishika nafasi ya pili na mwigizaji maarufu wakati huo, Bakari Mbelemba, maarufu kama Mzee Jangala akakamata nafasi ya tatu.

Remmy, ambaye alijua atashinda kirahisi pambano hilo, hakukubali, akakata rufani kwa majaji kuwa mshindi wa kwanza Masudi hakuwa mbaya wa asili, bali ulitokana na kuugua ukoma.

Majaji waliichukua rufani yake na kuifanyia kazi. Kilichotokea ni kwamba rufani ya Dk. Remmy ilitupwa kwa kuwa ilionekana Masudi yuko vile tangu utoto wake. Kilichomuuma zaidi Dk. Remmy ni vyombo vya habari, hususan magazeti wakati ule, kuandika kuwa Remmy pamoja na ubaya wake kwa Masudi alionekana mrembo tu.

Ilimuuma sana kwa kuwa aliamini hakuna mtu mwenye sura mbaya nchini Tanzania kama yeye na akaimba nyimbo nyingi za kujisema kama yeye ni mbaya kama 'mtoto ni mtoto kwa mama hakui, hata kama angelikuwa kilema au mbaya kama Remmy, ni mtoto tu.' Wimbo huo unaitwa 'Nalilia Mtoto'. Wimbo mwingine ni 'Mnyonge hana haki', kuna kipande anaimba 'Remmy myonge, Remmy sura mbaya, Remmy hana la kusema mbele ya wenzake.'

Alijitahidi sana kutaka kuandaa tena mara ya pili kwa kuwa alijua atashinda lakini ilishindikana kwa sababu alianza kuugua na alipopona, akaamua kuokoka.

Cha ajabu ni kwamba pamoja na kumkataia rufani, Remmy alianza kumtumia Masudi Surambaya kwenye maonyesho yake. Sitaki kuendelea sana na hili kwa sababu tayari tumeshalizungumza, ila nimegusia kumwonyesha Remmy alivyokuwa nje ya muziki.

Ni mtu mwenye vituko, na anapopita iwe kwa miguu au ndani ya gari, lazima watu wajue kama anapita.

Mavazi yake, nywele zake aina ya rasta, zilikuwa kivutio ukichanganya na umaarufu wake ndiyo kabisa. Ndiyo maana kuna wimbo aliimba, 'Remmy akipita barabarani' watoto humfuata'. Ni kweli kabisa.

Hakuwa mtu wa majivuno, alikuwa rafiki na kipenzi wa kweli wa mashabiki, kwani wao walimpa upendo na yeye akalipa kwa kuwapa faraja kwa kuongea na kucheka nao.

Kituko ambacho hakijawahi kuelezewa sana ni gari lake. Sijui alilinunua kwa bahati mbaya au makusudi ili tu avunje mbavu watu. Muundo wa gari ile sina uhakika kama lilikuwa 'Morris' au 'Austin'. Yale magari ya kizamani kabisa, ambayo kwa miaka ya 1980, yalionekana yamepitwa na wakati.

Ni kipindi Tanzania ilishuhudia magari mpya kama Renault na Peugeot, hasa 504 maarufu kama 'guruwe' ndiyo yalikuwa yameingia na ndiyo ya kisasa.

Gari la Remmy likionekana barabarani lilionekana ni kituko na yeyote anayeliona ataanza kulishangaa kwa kulikodolea macho au kucheka. Mwenyewe alijua hilo. Nyuma ya gari hilo aliandika maandishi yaliyosomeka 'Baba yako analo?' Unapolicheka, ukisoma maandishi nyuma, utaacha kucheka na kujiuliza maswali, au atazidi kuvunjika mbavu kutokana na kushuhudia kichekesho juu ya kichekesho.

Baadaye alinunua gari lingine halitofautiani sana na hilo lakini akaandika 'sukari imeingia sumu, mambo kwa soksi.' Yalikuwa maandishi yaliyowatahadharisha watu kuhusu ugonjwa hatari wa UKIMWI, wakati huo ndiyo ulikuwa imeingia na wengi hawana uelewa. Alikuwa akiwakumbusha juu ya kutumia mipira ya kiume, maarufu kamka kondomu.

Kwa upande wa watoto walimpenda Remmy kwa sababu alikuwa akiwapa sana lifti kwenye gari Lake.

Akipita kituoni na kukuta wanafunzi hasa watoto kuanzia wanaosoma chekekea na shule za msingi, atasimama na kuwapakiza mpaka gari lake lijae. Yeye huwaambia 'Pandeni niachieni' kitu changu tu'.

Hiyo ilikuwa ndiyo tabia yake popote pale anapopita. Kumbuka watoto hawa huwa wanakwenda kuwaambia wazazi wao majumbani juu ya kupewa lifti naye. Ndiyo maana umaarufu wa Remmy ulikuwa mkubwa maradufu. Si kwa ajili ya muziki tu peke yake. Roho yake ya upendo, huruma, ukarimu, kujiweka karibu na mashabiki wake, kutokuwa na maringo, licha ya kuwa ni staa mkubwa ndani ya nje ya nchi, ilimfanya kupendwa na kuheshimiwa zaidi.

Mwanamuziki huyo alifariki dunia Desemba 13, 2010 na kuzikiwa kwenye makaburi ya Sinza, eneo ambalo aliokuwa akiishi tangu kukiwa pori mwanzoni mwa miaka ya 1980, kiasi kwamba hadi leo sehemu hiyo imepewa jina lake kwa heshima yake tangu yuko hai hadi alipofariki dunia. 'Sinza kwa Remmy'.

**Kwa maoni tuma 0716 350534**

# HADITHI

# Ajenda ya Siri-5

TINA, msichana kutoka Mpanda, mkoani Katavi anafiwa na wazazi wake wote wawili kwa ajali ya gari akiwa na miaka 10 tu. Tabu alizozipata kutokana na kunyanyaswa na ndugu zake, zilimfanya kuishi maisha ya mateso. Hata shule aliishia la saba tu. Alipofikisha umri wa miaka 18 akakimbilia Dar es Salaam na kuanza kufanya kazi za ndani. Baadaye akabahatika kupata kazi za ndani kwa mfanyabiashara mmoja maarufu, Hafidh Chilambo. Mfanyabiashara huyo anafariki kwa kula chakula kilichowekwa sumu. Chakula hicho kilipikwa na Tina. Mahakama Kuu inamhukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Je ni wafanyabiashara wenzake Chilambo ndiyo waliomtuma msichana huyo kwa kumwahidi mamilioni ya pesa kutokana na ugomvi wa kibiashara? Au ni kwa sababu hajalipwa mshahara wake wa miezi sita aliokuwa anadai? Fuatilia kila nakala ya Nipashe ili kuupata ukweli ulio nyuma ya pazia wa sakata hili.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

USHAHIDI ulioendelea mahakamani ulieleza kuwa uchunguzi wa awali ukionyesha kuwa alifariki baada ya kula chakula ambacho kilikuwa na viashiria vya sumu. Kabla ya mazishi, daktari Thomas Mtuta aliuchunguza mwili ya marehemu na kugundua kuwa ndani ya chakula alichokula, kuliwekwa aina mbili za dawa baridi ambazo si chungu, lakini zikichanganywa na mtu akinywa kwa kuwekewa kwenye kinywaji, au chakula, basi anaweza kupoteza maisha masaa mawili au matatu baada ya kunywa, na athari zinaanza kuonekana kiasi cha nusu saa tu baada ya kuingia mwilini.

Mshtakiwa mwenyewe alikiri vyote, lakini alijitetea kuwa hakujua kama chakula hicho kina sumu au dawa yoyote iliyowekwa.

Alipoulizwa kwa nini sio yeye wakati siku hiyo alikuwa yuko peke yake kuanzia saa nne asubuhi, alishindwa kujibu.

Mfamasia Mwahija Chota, yeye alikuwa mmoja wa mashahidi upande mashtaka aliiambia mahakama kuwa siku hiyo ambayo inayotajwa kuwa Hafidh Chilambo alifariki kwa kula chakula chenye sumu, mshtakiwa Tina alifika kwenye duka na kununua aina mbili za dawa.

Mwahija aliionyesha mahakama daftari lake ambalo huandika dawa ambazo huuza. Aina hizo ni moja ya dawa zilizouzwa siku hiyo. Daftari lilionyesha kuwa ziliuzwa saa tano na robo. Robo saa tu, baada ya muda ambao Tina aliondoka nyumbani.

Ni aina hizo hizo za dawa ambazo daktari Mtuta alisema zilionekana kwenye mwili wa marehemu ulipofanyiwa uchunguzi.

Kutokana na ushahidi wote huo, huku upande wa utetezi ukishindwa kabisa kukabiliana na ule wa upande wa mashtaka, mahakama ikatoa huku hiyo.

Hapo ndipo Eddy alipoelewa moja hadi mwisho wa kesi jinsi ilivyoendeshwa hadi msichana Tina Kauzeni alipohukumiwa kunyongwa hadi kufa.

Hakuwa na cha kuongeza. Kila kitu kilikuwa sawa. Lakini kwa akili yake ya kawaida alijiuliza kama Tina alifanya hivyo kwa sababu gani "Ni lazima kuwe na kisa. Hiki mimi ndiyo nakitaka." Alijiambia mwenyewe.

Kuhusu kunyimwa mshahara kiasi cha miezi sita, hilo alikuwa ameshalifunga mjadala, kwani walezi wake kina bi Mtupeni ameshakataa na kusema kuwa sio yeye tu aliyekuwa analipwa, bali hata wao walikuwa wanachukua posho kila mwisho wa mwezi kwa kuwapa binti huyo.




**Mwahija aliionyesha mahakama daftari lake ambalo huandika dawa ambazo huuza. Aina hizo ni moja ya dawa zilizouzwa siku hiyo. Daftari lilionyesha kuwa ziliuzwa saa tano na robo. Robo saa tu, baada ya muda ambao Tina aliondoka nyumbani.**

"Je hili la wafanyabiashara wenzake kumtumia binti huyu kumuua mwenzao linaweza kuwa na ukweli?" Aliendelea kujiuliza. Halafu akajijibu "Lakini mzee Digalu na mkewe walikataa na kusema hawakuona mabadiliko yoyote ya kuongezeka kwa pesa kwa binti yao. Je kuna kweli? Au waliniongopea? Au kwa sababu ni binti mdogo wafanyabiashara wakampa pesa ndogo tu kama kianzio, halafu akitekeleza mauaji basi watamlinda na kumpa zilizobaki?" Lilikuwa ni lundo la mawazo alikokuwa nalo Eddy.

Alijikuta akitoa simu yake ya mkononi na kumpigia wakili Tinga.

"Una muda rafiki yangu?" Alimuuliza.

"Saa nane nitakuwa na muda." Tinga alijibu.

"Nakuomba basi uje ofisini, ni muhimu sana."

"Poa, nitafika."

********************************

"Uliusoma mtiririko wa ile kesi ya yule binti niliyokutumia?" Wakili Tinga alimuuliza, baada ya utani mwingi alipoingia ofisini mwa Eddy Kamal.

"Ndiyo nilichokuitia hicho. Unadhani nimekuitia msosi?" Alitania.

"Nilijua tu ni masuala ya kazi, msosi ungeniitia huku ofisini ndugu yangu?"

"Sasa ni hivi. Mimi nimesoma nimeelewa. Ushahidi wote uneonekana ni kweli binti ametenda kosa hilo na anastahili adhabu ile, lakini hapa naona kuna watu ambao wamejificha nyuma ya hili." Eddy alimuweka wazi rafiki yake.

"Ni kweli, lakini hakuna sehemu yoyote ambayo wametajwa, wala upande wa utetezi haukusema kuwa ulitumwa na mtu." Alisema wakili Florence Tinga.

"Ndiyo, na ukumbuke kuwa hata Tina mwenyewe mpaka anahukumiwa hakusema kuwa amefanya hilo tukio, ni ushahidi ndiyo umemfunga."

"Ni kweli Eddy."

"Unaamini kweli binti anaweza kufanya lile tukio kwa akili yake. Mwenyewe tu, aamue, amuue baba wa watu bila kisa. Tena ingekuwa mkewe Hellen sana, kwa sababu hawa baadhi ya kinamama wakati mwingine wakikaa na madada wa kazi kunakuwa na matatizo kidogo, lakini baba anaye toka asubuhi na kurudi jioni, mara nyingi wanakuwa hawana matatizo yoyote nao."

"Nimekuelewa Eddy, sasa kwani unachotaka kufanya wewe ni nini?"

"Kuingia kazini." Alijibu. Ni maneno mawili tu ambaye Eddy aliyasema, lakini kwa wakili Tinga yalikuwa na maana kubwa. Anamjua Eddy. Ni mmoja wa wapelelezi maarufu nchini Tanzania. Umaarufu wake ni kupeleleza visa, mikasa, au mambo yaliyoshindikana na yaliyojificha. Alichukuliwa kama si mpelelezi wa kawaida. Ameshawahi kuifanyia nchi mambo mengi muhimu na kufichua mafisadi, majambazi, wahaini na watu wengine wenye nia mbaya na nchi. Lakini pia amekuwa akijiingiza mwenyewe kwenye visa, mauaji na mikasa ya kijamii ambayo imeshindikana kwenye uchunguzi wa kawaida.

"Eeeh!. Unataka kuingia kwenye hili sakata?" Alijikuta akiuliza kwa mshangao.

"Mbona kwako ni dogo sana, halafu hukumu imeshatoka na ushahidi uko wazi kabisa kuwa binti amefanya tukio hilo?"

"Ndiyo, lakini nataka kuwapata wale waliomtuma."

"Mmhh, sawa kwa wewe nakuamini, ila naona kama utajichosha."

"Hapana, hii ngoma naingia mwenyewe kuicheza, nataka kumpata mtu yeyote ambaye yuko nyuma ya mpango huu. Lazima kuna mtu amemshinikiza au kumshawishi yule binti. Kama binti yule anakwenda kunyongwa, halafu kuna mtu au watu waliomtuma watakuwa wakikaa hotelini, au kwenye baa wanagongeana glasi kwa kushangilia Hafidh Chilambo waliotaka auawe wamefanikiwa, sitokuwa radhi nao." Sauti ya Eddy sasa ilibadilika ilikuwa ni ya kimamlaka zaidi.

"Kesho nitamuona mkuu wangu wa kazi anipe kibali cha kuanza kazi hii?" "Okay, kumbe huwa hamfanyi tu hivi hivi?"

"Hapana, ni lazima niwasiliane na bosi wangu, Mkuu wa Idara wa Usalama, na aniandikie barua ya kukubali ninachotaka kufanya, na hicho kinakuwa ni kuruhusu kwenda popote, kumfuata yeyote, kumhoji mtu yeyote, kuingia sehemu yoyote ile na wakati mwingine kufanya chochote, ikiwamo hata kujeruhi au kuua kama ikihitajika au kushindikana kwa hali ya kawaida."

"Sawa, mimi sikupingi kwa hilo."

"Kama watakuwa ni wafabiashara wenzake kwa sababu ya kudhulumiana, basi ninachotaka wajulikane ili nao wapelekwe mahakamani wakapate stahiki. Wakati Tina ananyongwa, basi na wao wakamatwe wapate adhabu inayowafaa. Na kama siyo wafanyabiashara, ila kuna mtu amemtuma tu kwa sababu zake au kikundi chochote kwa sababu zao tu, basi sitokubali kabisa kiwe uraiani. Nitawatafuta popote pale, ikiwezekana hata kuingia chini ya ardhi, ili wapatikane. Kuanzia wiki ijayo naanza kazi hiyo."

"Hakuna tatizo, nakutakia kazi njema, ila kama kuna kitu utakuwa unahitaji cha kisheria zaidi, basi usisite kunipigia, njoo ofisini au niite kama kawaida tu."

"Hilo halina shaka." Eddy alijibu. Tinga alinyanyuka na kupenana mikono tena kama walivyofanya wakati alipowasili."

**INAENDELEA JUMAPILI**

HABARI BURUDANI



# BABU TALE
## AWASIMANGA VIHEREHERE

MENEJA wa WCB na Mbunge wa Morogoro Kusini, Babu Tale, amesema Watanzania waache dhana kwamba msanii kutoka kimuziki lazima asaidiwe.

Amesema watu wasiwafuate wagombanishi wachache ambao wanaweza kuua muziki kutokana na maneno yao ya kuponda wanamuziki.

"Ningekuwa na uwezo ningewasimamisha watu kama hawa wasifanye kazi katika vyombo vya habari, watu wa aina hii hawapo Kenya, Rwanda hata Nigeria, ni lazima tuwe makini nao," amesema Babu Tale.



# KAUSIME
## KUICHEKESHA DAR DISEMBA

MTANGAZAJI nguli nchini Zamaradi Mketema , anatarajia kumdondosha mchekeshaji mkongwe, Anne Kansiime kutoka Uganda katika tukio kubwa la ucheshi, December To Remember.

Akizungumza na Nipashe, Zamaradi alisema tukio hilo la ucheshi wima (Standup Comedy) litakafanyika Desemba 4, mwaka huu katika viwanja vya Gymkhana kuanzia saa moja usiku.

"Tumeiita 'December To Remember' sababu ni siku ya kukumbukwa kwa kile ambacho kitakwenda kufanyika kwenye tasnia ya uchekeshaji hapa nchini, lengo watu wacheke kwenye viwango vya kimataifa, kwahiyo mbali na Kansiime wa Uganda, kutakuwa na wachekeshaji wengine wakubwa kutoka hapa Tanzania, watu wajiandae kuburudika," amesema Zamaradi.

## Hakika thubutu kafanye ukione cha moto



WAKATI baadhi ya mastaa wa kike nchini, wanapigana vikumbo kufanya upasuaji wa kurekebisha viungo, mchekeshaji Hakika Ruben, amewashangaza wengi baada naye kuahidi kufuata tiba hiyo ili afanane na Wema Sepetu.

Hakika amesema anataka kufanya upasuaji wa utumbo ili kupunguza tumbo na kutaka mwonekano mwembamba kama Wema Sepetu, ambaye anadaiwa kufanya hivyo miaka ya hivi karibuni.

"Sura mwanzoni sikuwa nayo, nimetumia dawa kuongeza weupe na mwezi unaokuja nakwenda China kupunguza utumbo nataka kuwa mwembamba," amesema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### POGBA RUKSA KUONDOKA

KLABU ya Manchester United inapanga kumwachia kiungo wa kati, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 28, aondoke huku akiwa na uwezekano mkubwa wa kwenda Real Madrid. **(Marca via Sport Witness)**

### LINGARD ANUKIA WEST

KIUNGO wa kati wa Manchester United na England, Jesse Lingard (28), huenda akawa njiani kuelekea West Ham Januari mwakani kwa mkataba wa pauni milioni 10. Mazungumzo ya mkataba baina ya United na mchezaji huyo yalivunjika hivi karibuni. **(Sun)**

### CONTE AMTAKA LINGARD

KOCHA wa Tottenham, Antonio Conte, ameweka wazi nia ya kumsajili kiungo, Jesse Lingard, kutoka Manchester United kwa uhamisho wa bila malipo msimu ujao. **(Express)**

### TRIPPIER ATAKIWA UNITED

MANCHESTER United wana nia ya kumsajili, Kieran Trippier kutoka Atletico Madrid. United wanajiandaa kumuuza Diogo Dalot mwenye miaka 22 kwa Roma iwapo Trippier (31), atajiunga na kikosi hicho. **(Manchester Evening News)**

### XAVI ATAKA MAJEMBE

WALINZI wa Chelsea, Cesar Azpilicueta na Andreas Christensen wanalengwa na Xavi ambaye anataka kuwasajili wawili hao kule Brcelona. Mikataba ya Azpilicueta, na Christensen mweye umri wa miaka 32, inamalizika msimu ujao. **(Express)**

### STARK KUTUA EPL

KLABU ya West Ham ina mpango wa kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Ujerumani na Hertha, Berlin Niklas Stark, mwenye umri wa miaka 26. **(Sport1 via Team Talk)**

### TARKOWSKI HAONDOKI

KOCHA wa Burnley, Sean Dyche amesema, James Tarkowski mwenye miaka 28, ana "mawazo ya wazi " na "malengo" licha ya kwamba klabu za Newcastle, West Ham na Tottenham zinamtaka. **(Burnley Express)**

### ELNENY SAFARI IMEIVA

ARSENAL wameafiki mkataba wa kumruhusu kiungo wa kati Timu wa Taifa ya Misri, Mohamed Elneny mwenye miaka 29, kujiunga na klabu ya Galatasaray. **(Vatan via Express)**

### PULISIC KUREJEA LIVERPOOL

WINGA wa Chelsea, Christian Pulisic, huenda akaelekea Liverpool kwani muda wa mchezo anaopewa Mmarekani huyo katika timu hiyo unaendelea kuwa mfupi. **(Star)**

### TOLISSO AGOMBEWA

TOTTENHAM Hotspur, imeonyesha nia ya kutaka kumsajili kiungo wa kati wa Bayern Munich na Ufaransa, Corentin Tolisso, lakini wanaweza kukabiliana na ushindani kutoka kwa Inter Milan ambao pia wanamhitaji mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27. **(Kicker)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# CITY YAJIPANGA KUMSAJILI DE JONG

●●●Ni baada ya kuwasilisha rasmi ofa kwa Barcelona licha ya Mholanzi huyo...

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester City imeripotiwa imewasilisha ofa rasmi ya euro milioni 90 kwa ajili ya kumsajili nyota wa Barcelona, Frankie de Jong.

De Jong amekuwa mchezaji muhimu wa Barcelona tangu alipowasili klabuni hapo mwaka 2019.

Hata hivyo, licha ya umuhimu wa De Jong, Barca kumekuwa na mawazo anaweza kuwekwa sokoni ili kupunguza changamoto ya kifedha klabuni hapo.

Uwepo wa Gavi na jitihada zake zinahatarisha hatima ya nafasi ya De Jong kwenye kikosi cha kwanza cha Barcelona ikiwa Pedri atarejea kutoka kuuguza majeraha.

Nyota huyo raia wa Uholanzi, atakuwa kama mchezaji wa ziada, na bila shaka anahitaji muda zaidi wa kucheza kwa upande wake.

Kwa mujibu wa chapisho la Fichajes, Manchester City walikuwa wakivutiwa na nyota huyo kwa muda sasa tangu alipokuwa Ajax, wamejaribu kuwasilisha ofa yao kwa Barcelona ya euro milioni 90.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Barcelona watakuwa tayari kumwachia De Jong aondoke, na kutengeneza faida ya pauni milioni 10.

## HABARI MICHEZO











# TOTTI AMTETEA MOURINHO ROMA

**ROME, Italia**

JOSE Mourinho sio tatizo kwenye kikosi cha AS Roma, klabu na mashabiki kwa pamoja wanapaswa kumuunga mkono, amesema gwiji aliyewahi kutamba na timu hiyo, Francesco Totti.

Roma walimteua Mourinho kuwa kocha tangu Mei, mwaka huu, na waliwekeza takribani euro milioni 130 kwa ajili ya wachezaji wapya.

Licha ya mambo kuanza vyema, Roma wakishinda mechi zao sita za msimu kwa mara ya tatu kwenye historia yao, wameshinda mechi nne pekee katika mechi 12 walizocheza ugenini.

Baada ya hapo kiwango cha Roma kikaanza kuporomoka na wakimaliza safari yao ya ushindi wa mechi 43 mfululizo za nyumbani.

Novemba pia haujawa mwema sana kwa Roma wakianza na kutoa sare nyumbani kabla ya kukubali kichapo cha 3-2 dhidi ya Venezia.

"Kama tukidhani tatizo la Roma ni Mourinho, inamaanisha kila kitu hakiko sawa kwetu," amesema Totti anikunukuwa na Sky Sport Italia.

"Saluti kwa Mourinho, ameshinda mechi nyingi zaidi ukifananisha na makocha wengine wote wa Serie A.

"Klabu na mashabiki wanapaswa kumuunga mkono, kwani bado ana nafasi ya kufanya vizuri zaidi."

# Garcia: Ninamwona Guardiola kwa Xavi



**BARCELONA, Hispania**

NYOTA Eric Garcia amemfananisha kocha mpya wa Barcelona, Xavi Hernandez na Pep Guardiola na Luis Enrique.

Garcia amefanya kazi chini ya Guardiola akiwa Manchester City, ambao aliachana nao na kurejea Barcelona.

Nyota huyo pia alifanya kazi na Enrique kwenye Timu ya Taifa ya Hispania.

Xavi ameanza majukumu mwisho mwa wiki iliyopita, lakini tayari joto la mabadiliko limeanza kuonekana Barcelona.

Kwa mujibu wa Garcia, Xavi ni mtu sahihi kuiongoza Barcelona kwa sasa.

"Ni mtu sahihi kuiongoza Barcelona. Kwa Xavi ninaona vitu kutoka kwa Pep (Guardiola) na Luis Enrique pia. Ni gwiji wa timu na kocha mzuri," amesema Garcia akinukuliwa na Marca.

Lakini pia Garcia alimzungumzia mtangulizi wa Xavi kuwa kwa upande wake alimsaidia katika vitu mbalimbali mpaka alipofikia sasa.

Akimzungumzia, Ronald Koeman alinukuliwa akisema: "Kwa upande wangu, alinisaidia sana na sina maneno zaidi ya kusema asante."

Kibarua rasmi cha Xavi kilianza jana Jumamosi wakati kikosi chake kilipokutana na Espanyol.

LIVE IN PLAY

# TANZANIA YAIPANIA MSUMBIJI FAINALI YA UFUKWENI COSAFA

**Na Saada Akida**

TIMU ya Soka ya Taifa ya ufukweni inatarajia kuwakabili wenzao kutoka Msumbiji katika mchezo wa fainali ya mashindano ya COSAFA utakaochezwa leo kwenye ufukwe wa South Arena, jijini Johanesburg nchini Afrika Kusini.

Tanzania inacheza fainali hiyo baada ya kumfunga Angola mabao 5-2 katika mechi ya hatua ya nusu fainali, na itakutana kwa mara ya pili na Msumbiji kutokana na kucheza mchezo wa ufunguzi wa michuano hiyo.

Katika mchezo wa kwanza Tanzania ilipokutana dhidi ya Msumbiji ilishinda penalti 4-3 baada ya kumalizika dakika 90 kwa sare ya mabao 4-4. Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Tanzania, Boniface Pawasa, alisema wamefanyia kazi upungufu wao na wamejipanga kuhakikisha wanafanya vizuri katika mchezo huo wa fainali.

Pawasa alisema ana matarajio makubwa ya kuibuka mabingwa kwa sababu lengo lao kubwa lilikuwa ni kuipeperusha vyema bendera ya Tanzania katika michuano hiyo.

"Ni jambo la kumshukuru Mungu kufikia hatua hii, Msumbiji ni wapinzani wetu tumekutana katika mchezo wa ufunguzi na kutoka sare, tunawaheshimu na tumeyafanyia kazi madhaifu yetu, tunafahamu ubora wao, tunajua utakuwa mchezo wa ushindani mkubwa kwa pande zote mbili," alisema Pawasa.

Aliongeza kikosi chake kipo vizuri kuelekea fainali hiyo na hakuna majeruhi hata mmoja na kilichobakia ni wachezaji kutimiza majukumu yao ya uwanjani.

"Tuna kila sababu ya kupambana ili kufanya vizuri katika michuano hii ya COSAFA kwa upande wa mchezo wa soka la ufukweni. Tunataka kuendeleza pale walipofika dada zetu Twiga Stars," Pawasa aliongeza.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya ufukweni wakishangilia baada ya kuifunga Angola mabao 5-2 na kutinga hatua ya fainali ya mashindano ya Kombe la COSAFA ambayo yanatarajiwa kumalizika leo nchini Afrika Kusini. **PICHA: TFF**

# KMKM, Zimamoto, Malindi zaendeleza ubabe Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MABINGWA watetezi, KMKM wameendelea kujiimarisha kileleni baada ya kuichapa Kisiwani mabao 4-1 katika mechi ya Ligi Kuu ya PBZ Zanzibar iliyochezwa kwenye Uwanja wa Gombani, Pemba juzi.

Kwa matokeo hayo, 'Maafande' hao wa KMKM wamefikisha pointi 16 baada ya kucheza michezo na kuufanya huo kuwa ushindi wao wa tano na sare moja tangu kuanza msimu huu.

Nafasi ya pili ya msimamo wa ligi hiyo inashikiliwa na Wekundu wa Mji Mkongwe, Malindi ambapo wamefikisha pointi 14 baada ya kuifunga Mlandege magoli 2-1 mchezo uliofanyika Uwanja wa Amaan.

Zimamoto yenye pointi 12 inashika nafasi ya tatu katika msimamo wa ligi inayoshirikisha timu 16 baada ya kuifunga Taifa Jang'ombe goli 1-0, Uwanja wa Gombani.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa KMKM, Ame Msimu, alisema ligi ya msimu huu ni ngumu na yenye ushindani zaidi ukilinganishaa na misimu mingine iliyopita.

Alisema ugumu wa ligi hiyo umetokana na udhamini uliopatikana ambapo kila timu inapambana kuhakikisha inanyakua ubingwa na kupokea kitita za zawadi ya Sh. milioni 50 itakayotolewa.

Wadhamini wakuu wa ligi hiyo ni Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), ambao pia wameahidi kutoa Sh. milioni 30 kwa timu itakayochukua ubingwa wa Kombe la FA.

SPORTPESA APP

BET LEO UWE MILIONEA




MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 21 - NOVEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 3715 | Rostov vs Ufa | 1.78 | 3.44 | 4.42 |
| 14:15 | 5035 | GO Ahead Eagles vs Groningen | 2.27 | 3.33 | 2.94 |
| 14:30 | 4619 | Sassuolo vs Cagliari | 1.64 | 4.22 | 4.72 |
| 15:00 | 1761 | Derby vs Bournemouth | 4.51 | 3.43 | 1.76 |
| 15:00 | 2335 | Brest vs Lens | 3.08 | 3.42 | 2.23 |
| 15:30 | 3742 | Anderlecht vs Kortrijk | 1.40 | 4.75 | 6.73 |
| 16:00 | 3000 | Konyaspor vs Caykur Rizespor | 1.70 | 3.66 | 4.65 |
| 16:00 | 5708 | Getafe vs Cadiz CF | 1.96 | 3.10 | 4.40 |
| 16:30 | 2630 | Feyenoord vs PEC Zwolle | 1.19 | 6.49 | 11.79 |
| 16:30 | 2807 | Dinamo Moscow vs Arsenal Tula | 1.41 | 4.44 | 6.90 |
| 16:30 | 5476 | Austria Klagenfurt vs Austria Vienna | 2.80 | 3.33 | 2.26 |
| 17:00 | 2565 | Strasbourg vs Reims | 1.97 | 3.28 | 3.97 |
| 17:00 | 2950 | Bologna vs Venezia | 1.62 | 4.10 | 5.01 |
| 17:00 | 3470 | Troyes vs St Etienne | 2.34 | 3.37 | 2.93 |
| 17:00 | 3908 | Angers vs Lorient | 1.85 | 3.49 | 4.19 |
| 17:00 | 4112 | Metz vs Bordeaux | 2.40 | 3.24 | 2.94 |
| 17:00 | 4376 | Salernitana vs Sampdoria | 2.99 | 3.28 | 2.38 |
| 17:00 | 5323 | Manchester City vs Everton | 1.20 | 6.47 | 13.99 |
| 17:30 | 4362 | SC Freiburg vs Eintracht Frankfurt | 2.05 | 3.54 | 3.39 |
| 18:00 | 1403 | Copenhagen vs Aarhus | 1.81 | 3.55 | 4.14 |
| 18:00 | 5844 | St Truiden vs Royal Antwerp | 2.71 | 3.40 | 2.43 |
| 18:15 | 2900 | Granada vs Real Madrid | 5.51 | 4.27 | 1.55 |
| 18:30 | 1257 | FC Lugano vs FC Luzern | 2.00 | 3.46 | 3.51 |
| 18:30 | 5575 | Maritzburg Utd vs Kaizer Chiefs | 3.18 | 2.99 | 2.32 |
| 18:45 | 2368 | Waalwick vs Ajax | 17.61 | 8.42 | 1.11 |
| 19:00 | 2201 | Stabaek vs Kristiansund | 2.86 | 3.41 | 2.31 |
| 19:00 | 2322 | Bodo Glimt vs Lillestrom | 1.39 | 4.93 | 6.51 |
| 19:00 | 3005 | Galatasaray vs Fenerbahce | 2.16 | 3.35 | 3.20 |
| 19:00 | 3441 | Rangers vs Hibernian | 1.45 | 4.15 | 5.98 |
| 19:00 | 4543 | Sarpsborg vs Odd Ballklubb | 1.98 | 3.59 | 3.44 |
| 19:00 | 4600 | Adanaspor vs Ankaragucu | 3.41 | 3.37 | 1.96 |
| 19:00 | 5377 | Clermont Foot vs Nice | 3.43 | 3.43 | 2.08 |
| 19:00 | 5616 | Valerenga vs Tromso | 1.85 | 3.60 | 3.89 |
| 19:30 | 2395 | Tottenham vs Leeds | 1.69 | 4.00 | 4.60 |
| 19:30 | 3900 | Varbergs Bois vs AIK Football | 3.08 | 3.03 | 2.24 |
| 19:30 | 5481 | Mainz vs FC Koln | 2.11 | 3.57 | 3.22 |
| 19:30 | 5850 | Sochi vs Rubin Kazan | 1.65 | 3.72 | 4.90 |
| 20:00 | 2617 | Midtjylland vs Brondby | 1.72 | 3.83 | 4.32 |
| 20:00 | 5535 | Inter vs Napoli | 2.23 | 3.46 | 3.11 |
| 20:30 | 1020 | Desna Chernigov vs Kolos Kovalivka | 2.02 | 3.33 | 3.28 |
| 20:30 | 1067 | Elche vs Betis | 3.46 | 3.31 | 2.13 |
| 20:30 | 1194 | Oostende vs Union Saint Gilloise | 5.31 | 4.33 | 1.52 |
| 20:30 | 3033 | Atromitos vs PAOK | 6.11 | 3.89 | 1.53 |
| 20:30 | 3336 | AEK Athens vs Olympiakos | 3.11 | 3.20 | 2.27 |
| 21:30 | 3231 | Steaua Bucuresti vs Botosani | 1.76 | 3.58 | 4.32 |
| 22:00 | 3021 | Cambuur vs Utrecht | 3.87 | 3.87 | 1.77 |
| 22:45 | 1329 | Genoa vs Roma | 4.51 | 4.11 | 1.68 |
| 22:45 | 5941 | Lyon vs Marseille | 1.91 | 3.88 | 3.53 |
| 23:00 | 2540 | Real Sociedad vs Valencia | 1.73 | 3.70 | 4.70 |
| 23:00 | 4686 | Kfco Wilrijk vs Racing Genk | 4.24 | 3.95 | 1.71 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumapili Novemba 21, 2021
Nipashe



City Yajipanga kumsajili De Jong

HABARI UK 21

## Simba yafunguka ilivyoimaliza Ruvu

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba, Pablo Franco, amesema pointi tatu walizopata katika mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara dhidi ya Ruvu Shooting ni muhimu na zimewaongezea wachezaji wake hali ya kujiamini kuelekea michezo inayofuata ikiwamo wa Kombe la Shirikisho Afrika.

Mhispania huyo amesema matokeo hayo pia yatawasaidia kujiimarisha kuelekea katika mechi dhidi ya watani zao, Yanga itakayochezwa Desemba 11, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Pablo alisema kikosi chake kilicheza vizuri hasa kipindi cha kwanza walivuna mabao yote matatu kwenye mchezo huo uliomalizika kwa ushindi wa 3-1.

Pablo alisema Simba ni timu kubwa na inastahili kupata zaidi ya walichokipata katika mechi yake hiyo ya kwanza ya mashindano tangu aliporithi mikoba ya Didier Gomes.

"Kwetu ulikuwa mchezo muhimu, kabla ya mechi nilizungumza na wachezaji na kuwaambia kwangu huu ulikuwa ni muhimu zaidi licha ya siku chache zijazo tutakuwa na mechi ya Kombe la Shirikisho, halafu tutakutana na Yanga, lakini mchezo huu ulikuwa muhimu kwa ajili ya kurudisha hali ya kujiamini,".

"Ni ushindi muhimu tulioupata, tunajua utaongeza morali kuelekea katika mchezo wetu wa hivi karibu wa kimataifa dhidi ya Reds Arrows ambao tutaanzia nyumbani na kuhitaji matokeo mazuri katika mchezo huo," alisisitiza Pablo.

Kocha huyo aliwapongeza wachezaji wake kuonyesha kiwango cha juu na ni matarajio yake kuona wanazidi kuimarika na wanaendelea na ubora huo kwenye michezo inayofuata.

"Kipindi cha pili, nafikiri kuna kitu au kazi ya kufanya. Tulijitahidi kumiliki mpira, hatukufunga, lakini tukaruhusu bao, tumekosa magoli na penalti pia. Hii itatufanya kufanya kazi kubwa kuyafanyia kazi mapungufu," alisema kocha huyo.

Naye Kocha Msaidizi wa Ruvu Shooting, Rajab Mohamed, alisema timu yao ilifungwa mabao matatu kipindi cha kwanza baada ya 'kufeli kwa plani' yao ya kwanza ambayo ilitokana na Simba kucheza tofauti na wanavyoifahamu.



Beki wa Yanga, Djuma Shabani (kulia), akijiandaa kumtoka winga wa Namungo FC, Shiza Kichuya katika mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Ilulu, mkoani Lindi jana. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA CHUPUCHUPU

## ●●●Yalazimisha sare dhidi ya Namungo FC, huku Geita Gold ikipata ushindi...

**Na Adam Fungamwango**

REKODI ya ushindi wa asilimia 100 wa Yanga ilikoma baada ya kukubali kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Namungo FC katika mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Ilulu, Lindi.

Vinara hao wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara walisubiri dakika kumi kabla ya kumalizika kwa mechi, waliposawazisha kwa penalti kupitia kwa mtokea benchi, Mrundi, Saido Ntibazonkiza.

Penalti hiyo ilitolewa mwamuzi, Abel William kutoka Arusha baada ya kiungo wa Yanga, Feisal Salum kuangushwa ndani ya eneo la hatari.

Kabla ya hapo Yanga ilikuwa nyuma kwa bao lililofungwa na straika wao wa zamani, Mzambia Obrey Chirwa.

Inakuwa ni sare ya kwanza ya Yanga msimu huu, huku ikiendelea kupunga upepo kileleni ikiwa na pointi 16, lakini sasa ikiizidi Simba pointi mbili tu, baada ya watani zao wa jadi kushinda mabao 3-1 kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza ilipokutana na Ruvu Shooting hapo juzi. Hata hivyo, Namungo itabidi ijilaumu yenyewe, kwani ndiyo iliyopata nafasi nyingi zaidi za wazi za kufunga mabao kwenye mechi hiyo kuliko Yanga, ambayo haikuwa kwenye kiwango chao cha kawaida ilichoanza nacho msimu huu.

Mechi ilianza kwa timu zote kupiga mipira mirefu ya juu, kitu kilichoondoa ladha ya mchezo wenyewe, ingawa Yanga ilikuwa ikipiga pasi fupi fupi nyuma na ndefu ikifika katikati, lakini Namungo ilitumia mipira mirefu kwa kipindi chote cha kwanza.

Dakika 18 za mwanzo hakukuwa na shambulio lolote, na ilipofika dakika ya 19 na 21, Namungo ilifanya mashambulizi kwenye lango la Yanga ambayo yangeweza kuipatia mabao, lakini Shiza Kichuya hakuwa na utulivu.

Kichuya aliyemegewa pasi ndefu na Lucas Kikoti, akiwa ndani ya eneo la hatari alipiga shuti lililogonga mwamba wa juu ya kurejea uwanjani na dakika mbili baadaye, alikosa tena bao lililokuwa rahisi zaidi kupata kuliko kukosa.

Ilikuwa ni kazi nzuri iliyofanywa na Relliants Lusajo aliyemhadaa Kibwana Shomari na kupiga shuti kali lililotemwa na kipa Djigui Diarra. Akiwa peke yake na goli, kipa akiwa ameanguka chini, hatua takriban tano tu kutoka golini, Kichuya, kwa mshangao wa wengi alipaisha juu.

Shambulizi pekee la hatari kwa Yanga kipindi cha kwanza, lilifanyika dakika ya 35, wakati Fiston Mayele alipopata mpira ndani ya eneo la hatari, alijikunja na kupiga shuti kwa mguu wa kushoto, ukatoka nje kidogo ya lango.

Hatimaye Chirwa aliandika bao dakika ya 52, alipowadanganya mabeki wa Yanga kama anatoa krosi, lakini aliufinya mpira, kabla ya kugeuka na kuachia shuti kali la pembeni, ambalo halikumshuhulisha hata kipa, Diarra kuruka.

Namungo iliendelea tena kukosa mabao ya wazi kupitia kwa Manyama dakika ya 69 na Kikoti dakika ya 73, kabla Yanga haijasawazisha bao na matokeo hayo yanaiweka Namungo kwenye nafasi ya 11, ikiwa na pointi sita.

Katika mechi ya mapema mchana, Mbeya City alimfunga Mtibwa Sugar mabao 3-1 huku Geita Gold akiwa ugenini alimchapa Kagera Sugar mabao 2-1.

Ligi hiyo inatarajiwa kuendelea tena leo kwa KMC kuialika Azam FC kwenye Uwanja wa Uhuru jijini.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042